**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# UCHAMBUZI WA UPIMAJI WA STADI ZA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU (KKK) DARASA LA PILI 2015

Kimetolewa na
Baraza la Mitihani la Tanzania
S.L.P. 2624
DAR ES SALAAM

MACHI, 2016

*Kimechapwa na*
Baraza la Mitihani la Tanzania
S.L.P. 2624
Dar es Salaam

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2016**

Haki zote zimehifadhiwa

# YALIYOMO


ORODHA YA CHATI .... VII

ORODHA YA VIELELEZO .... VIII

DIBAJI .... XI

SURA YA KWANZA .... 1

SAMPULI, ZANA ZA UPIMAJI NA UCHAMBUZI WA TAKWIMU .... 1

1.1 UTANGULIZI .... 1

1.2 SAMPULI YA UPIMAJI .... 1

1.3 ZANA ZILIZOTUMIKA KUFANYA UPIMAJI .... 2

1.4 UCHAMBUZI WA TAKWIMU .... 2

SURA YA PILI .... 4

UPIMAJI WA STADI YA KUSOMA .... 4

2.1 UTANGULIZI .... 4

2.2 MUUNDO WA KARATASI YA UPIMAJI WA KUSOMA .... 4

2.3 VIGEZO VYA UTENDAJI KATIKA STADI YA KUSOMA .... 5

2.4 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI .... 5

*2.4.1 Swali la 1: Kusoma Maneno .... 5*

*2.4.1.1 Wanafunzi Wanaojifunza kwa Lugha ya Kiswahili .... 9*

*2.4.1.2 Wanafunzi Wanaojifunza kwa Lugha ya Kiingereza .... 10*

*2.4.2 Swali la 2: Kusoma Sentensi .... 11*

2.4.2.1 WANAFUNZI WANAOJIFUNZA KWA LUGHA YA KISWAHILI .... 14

2.4.2.2 WANAFUNZI WANAOJIFUNZA KWA LUGHA YA KIINGEREZA .... 17

*2.4.3 Swali la 3: Ufahamu .... 18*

2.4.3.1 WANAFUNZI WANAOTUMIA LUGHA YA KISWAHILI KUJIFUNZIA .... 23

2.4.3.2 WANAFUNZI WANAOJIFUNZA KWA LUGHA YA KIINGEREZA .... 24

2.5 ULINGANIFU WA UMAHIRI KISHULE NA LUGHA YA KUFUNDISHIA .... 26

*2.5.1 Umahiri wa Wanafunzi kwa Shule za Mjini na Vijijini .... 26*

*2.5.2 Ulinganifu wa Umahiri kwa Wanafunzi Waliofanya Upimaji kwa Lugha ya Kiswahili na Kiingereza .... 27*

*2.5.3 Muhtasari wa Uchambuzi katika Stadi ya Kusoma .... 28*

SURA YA TATU .... 30

UPIMAJI WA STADI YA KUANDIKA .... 30

3.1 UTANGULIZI .... 30

3.2 MUUNDO WA KARATASI YA UPIMAJI WA KUANDIKA ........................................ 30

3.3 VIGEZO VYA UTENDAJI KATIKA STADI YA KUANDIKA KWA KILA SWALI ........ 31

3.4 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI ........................................ 31

*3.4.1 Swali la 1: Imla ........................................ 31*
*3.4.2 Swali la 2: Kutumia Herufi Kubwa kwa Usahihi katika Kuunda Maneno ...... 46*
*3.4.3 Swali la 3: Kunakili Kifungu cha Maneno na Kuweka Alama za Uandishi .. 50*

3.5 ULINGANIFU WA UMAHIRI KISHULE NA LUGHA YA KUFUNDISHIA ........................................ 53

*3.5.1 Umahiri kulingana na Lugha ya Kufundishia katika swali la 1 ........................................ 53*
*3.5.2 Ulinganifu wa Umahiri kwa Lugha ya Kufundishia katika Swali la 2 ........................................ 56*
*3.5.3 Ulinganifu wa Umahiri kwa Lugha ya Kufundishia katika Swali la 3 ........................................ 58*
*3.5.4 Ulinganifu wa Umahiri wa Stadi ya Kuandika kwa Kuzingatia Lugha ya Kufundishia na Maeneo Shule Zilipo ........................................ 59*
*3.5.5 Muhtasari wa Uchambuzi katika Stadi ya Kuandika ........................................ 62*

SURA YA NNE ........................................ 63

UPIMAJI WA STADI YA KUHESABU ........................................ 63

4.1 UTANGULIZI ........................................ 63

4.2 MUUNDO WA KARATASI YA UPIMAJI WA STADI YA KUHESABU ........................................ 63

4.3 VIGEZO VYA UTENDAJI KATIKA STADI YA KUHESABU ........................................ 63

4.4 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI ........................................ 64

*4.4.1 Umahiri wa Kutambua Namba Inayokosekana katika Mtiririko ........................................ 64*
*4.4.2 Umahiri wa Kujumlisha ........................................ 69*
*4.4.3 Umahiri wa Kutoa ........................................ 72*
*4.4.4 Umahiri wa Kufumbua Mafumbo ........................................ 76*

4.5 ULINGANIFU WA LUGHA YA KUFUNDISHIA NA MAHALI SHULE ILIPO ........................................ 83

*4.5.1 Umahiri kwa Kuzingatia Lugha za Kufundishia ........................................ 83*
*4.5.2 Umahiri wa Wanafunzi kutokana na shule ilipo ........................................ 86*
*4.5.3 Utendaji kwa Shule za Mjini na Shule za Vijijini ........................................ 88*
*4.5.4 Muhtasari wa Uchambuzi katika Stadi ya Kuhesabu ........................................ 90*

SURA YA TANO ........................................ 90

UCHAMBUZI WA TAARIFA ZA USIMAMIZI ........................................ 90

5.1 UTANGULIZI ........................................ 90

5.2 UJUZI WA KUFUNDISHA NA MAFUNZO YA WALIMU KATIKA STADI ZA KKK .. 90

5.3 MAHUDHURIO YA WANAFUNZI ........................................ 91

5.4 VIFAA, MAZINGIRA YA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ........................................ 92

SURA YA SITA ........................................ 94

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........................................94
6.1 HITIMISHO ........................................94
6.2 MAPENDEKEZO ........................................95
KIAMBATISHO NA 1: STADI YA KUSOMA ........................................97
KIAMBATISHO NA 2: READING SKILLS ........................................101
KIAMBATANISHO NA. 3: SKELI YA UPIMAJI ........................................105
KIAMBATANISHO NA. 4: ASSESSMENT SCALE ........................................110
KIAMBATISHO NA 5: STADI ZA KUANDIKA ........................................115
KIAMBATISHO NA 6: MANENO YA IMLA ........................................118
KIAMBATISHO NA 7: WRITING SKILLS ........................................120
KIAMBATISHO NA 8: DICTATION ........................................123
KIAMBATISHO NA 9: STADI YA KUHESABU ........................................125
KIAMBATISHO NA 10: ARITHMETIC SKILLS ........................................128
KIAMBATISHO NA 11: DODOSO LA MWALIMU MKUU ........................................130
KIAMBATISHO NA 12: DODOSO LA MSIMAMIZI MKUU ........................................132
KIAMBATISHO NA 13: DODOSO LA MWALIMU (MSIMAMIZI) ........................................134

## Orodha ya Majedwali


Jedwali Na 1: Idadi ya Wanafunzi Waliofanya Upimaji na Kuonesha Utendaji wa Wastani hadi Mzuri Sana ........ 3

Jedwali Na 2: Utendaji wa Wanafunzi katika Kusoma Maneno ........ 6

Jedwali Na 3: Utendaji wa Wanafunzi katika Kusoma Sentensi ........ 12

Jedwali Na 4: Utendaji wa Wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiswahili katika Kujibu Maswali ya Ufahamu ........ 23

Jedwali Na 5: Wanafunzi waliotumia lugha ya Kiingereza katika Kujibu Maswali ya Ufahamu ........ 25

Jedwali Na 6: Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Kunakili Kifungu cha Maneno na Kuweka Alama za Uandishi ........ 59

Jedwali Na 7: Utendaji wa Jumla wa Stadi ya Kuhesabu ........ 65

Jedwali Na 8: Wanafunzi Waliojibu Swali la 1 hadi 5 Usahihi ........ 66

Jedwali Na 9: Wanafunzi Waliojibu Swali la 6 hadi 10 kwa Usahihi ........ 70

Jedwali Na 10: Wanafunzi Waliojibu Swali la 11 hadi 15 Kwa Usahihi ........ 73

Jedwali Na 11: Wanafunzi Waliojibu kwa Usahihi Maswali ya afumbo ........ 77

Jedwali Na 12: Utendaji wa Wanafunzi katika Stadi ya Kuhesabu kwa Shule Zinazotumia Kiswahili ........ 83

Jedwali Na 13: Utendaji wa Wanafunzi kwa Shule Zinazotumia Kiingereza ........ 85

Jedwali Na 14: Utendaji wa Wanafunzi katika Shule za Mjini na Vijijini ........ 87

Jedwali Na 15: Utendaji katika Stadi ya Kuhesabu kwa Shule za Mjini na Vijijini ........ 89

Jedwali Na 16: Ufundishaji, Mafunzo na Muda Uliopangwa wa Upimaji  wa KKK ........ 91

Jedwali Na 17: Maoni ya Walimu Wakuu ........ 93

## Orodha ya Chati

Chati Na. 1: Wanafunzi walioweza Kusoma Maneno ........ 9

Chati Na. 2: Wanafunzi Walioshindwa Kusoma Maneno ........ 11

Chati Na. 3: Utendaji wa Wanafunzi katika Usomaji wa Sentensi ........ 17

Chati Na. 4: Asilimia ya Wanafunzi katika Usomaji wa Sentensi ........ 18

Chati Na. 5: Umahiri wa wanafunzi wa Shule za Mjini na Vijijini katika Upimaji wa Stadi ya Kusoma ........ 27

Chati Na. 6: Umahiri wa Wanafunzi wanaotumia Lugha ya Kingereza na Kiswahili ........ 28

Chati Na. 7: Umahiri wa Wanafunzi katika Uandishi wa Imla ........ 33

Chati Na. 8: Wanafunzi Walioshindwa Kuandika Maneno kwa Lugha ya Kiswahili na Kingereza ........ 46

Chati Na. 9: Ulinganifu wa Umahiri wa Wanafunzi Wanaotumia Lugha ya Kiswahili na Kiingereza Kujifunzia katika Kuandika Imla. ........ 55

Chati Na. 10: Ulinganifu wa Umahiri wa Wanafunzi katika Kuandika Herufi Kubwa kwa Kuzingatia Lugha ya Kufundishia ........ 57

Chati Na. 11: Ulinganifu wa Umahiri wa Wanafunzi katika Stadi ya Zilipo Kuandika kwa Kuzingatia Lugha ya Kufundishia na Maeneo Shule ........ 61

Chati Na. 12: Umahiri wa Wanafunzi Waliojibu Swali la 1 hadi 5 kwa usahihi ........ 66

Chati Na. 13: Wanafunzi Waliojibu Swali la 6 hadi 10 kwa Usahihi ........ 70

Chati Na. 14: Umahiri wa Wanafunzi waliojibu Swali la 11 hadi 15 kwa usahihi ........ 74

Chati Na. 15: Umahiri wa Wanafunzi Waliojibu kwa Usahihi Swali la 16 hadi 20 ........ 79

Chati Na. 16: Umahiri wa Wanafunzi katika Shule Zinazotumia Kiswahili ........ 84

Chati Na. 17: Umahiri wa Wanafunzi katika Shule Zinazotumia Kiingereza ........ 85

Chati Na. 18: Ulinganifu wa Umahiri kwa Shule za Mjini na Vijijini Zinazofundisha kwa Lugha ya Kiswahili ........ 88

Chati Na. 19: Umahiri wa Wanafunzi Utendaji kwa Shule za Mjini na Vijijini Zinazotumia Lugha ya Kiingereza ........ 90

Chati Na. 20: inaonesha utoro kuwa ndiyo sababu kubwa iliyofanya wanafunzi wasishiriki katika upimaji wa majaribio wa Darasa la Pili. ........ 92

## Orodha ya Vielelezo

Kielelezo Na. 1: Majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno kumi na tano (15) kwa muda wa dakika moja. ........................................................................................ 6

Kielelezo Na. 2: Majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno kumi (10) kwa muda wa dakika moja. ........................................................................................ 7

Kielelezo Na. 4: Majibu ya wanafunzi walioshindwa kusoma hata neno moja. .................. 8

Kielelezo Na. 3: Majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno matano (05) kwa muda wa dakika mbili........................................................................................ 8

Kielelezo Na. 5: Majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno 15 kwa dakika moja. . 12

Kielelezo Na. 6: Majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno kumi kwa dakika moja. ........................................................................................ 13

Kielelezo Na. 7: Majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno matano kwa dakika moja. ........................................................................................ 13

Kielelezo Na. 8: Majibu ya wanafunzi walioshindwa kusoma hata neno moja. ................ 14

Kielelezo Na. 9: Majibu ya wanafunzi walioweza kusoma habari na kujibu maswali yote manne kwa usahihi. ........................................................................................ 20

Kielelezo Na. 10: Majibu ya wanafunzi walioweza walioweza kujibu maswali matatu ya ufahamu ........................................................................................ 20

Kielelezo Na. 11: Majibu ya wanafunzi waliojibu maswali mawili ya ufahamu................. 21

Kielelezo Na. 12: Utendaji wa wanafunzi walioweza kujibu swali moja la Ufahamu. ........ 22

Kielelezo Na. 13: Majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali hata moja la Ufahamu. ........................................................................................ 23

Kielelezo Na. 14: Sampuli ya majibu ya wanafunzi wanaosoma katika shule zinazotumia Kiswahili/Kiingereza katika kufundishia walioweza kuandika maneno kumi kwa usahihi. 44

Kielelezo Na 15: Sampuli ya majibu ya wanafunzi wanaotumia Kiswahili/ Kiingereza kujifunzia walioweza kuandika maneno mawili ya Kiswahili na moja tu la Kiingereza kwa usahihi kati ya kumi. ........................................................................................ 45

Kielelezo Na. 16: Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kubadilisha maneno yaliyoandikwa kwa herufi ndogo kwa kuyaandika kwa herufi kubwa kwa usahihi............ 47

Kielelezo Na. 17: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeandika maneno kwa kuchanganya herufi kubwa na ndogo. ........................................................................................ 48

Kielelezo Na. 18: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeandika maneno yote kumi kwa herufi ndogo badala ya herufi kubwa. Aidha, mwanafunzi huyo katika baadhi ya maneno aliandika umbo "S" linaloonesha dhana ya wingi, jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya swali. .......................................................................................................... 49

Kielelezo Na. 19: Sampuli ya majibu ya wanafunzi walionakili kifungu cha maneno na kutumia alama za uandishi kwa usahihi. ...................................................................... 51

Kielelezo Na. 20: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweka alama za uandishi katika nafasi iliyoachwa wazi bila ya kunakili kifungu cha maneno. Aidha baadhi ya alama aliziandika kwa kugeuza kwa mfano alama ya kuuliza ? iligeuzwa na kuandikwa na alama ya mkato, iligeuzwa na kuandikwa ɕ. ............................................................... 52

Kielelezo Na. 21: Sampuli za majibu ya wanafunzi walioweka alama katika kifungu cha maneno bila kunakili. Aidha, wanafunzi hao hawakuweka alama hizo kwa usahihi. ........ 53

Kielelezo Na. 22: Mwanafunzi aliyejibu swali la 1 hadi 5 kwa usahihi katika dhana ya namba inayokosekana. ....................................................................................... 67

Kielelezo Na. 23: Mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi swali la 1 na 4 na kushindwa swali la 2, 3 na 5 katika dhana ya namba inayokosekana. ................................................................ 68

Kielelezo Na. 24: Mwanafunzi anayesoma katika shule inayotumia lugha ya Kiswahili kufundishia, aliyeshidwa swali la 8 na 9 yaliyohitaji kujumlisha namba kwa kubeba na swali la 10 lilihosu kujumlisha fedha. ...................................................................... 71

Kielelezo Na. 25 Mwanafunzi anayesoma katika shule inayotumia lugha ya Kiingereza kufundishia aliyeweza kujibu swali moja tu kwa usahihi lililohusu kujumlisha namba mbili zenye tarakimu moja bila kubeba. .......................................................................... 72

Kielelezo Na. 26: Mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi swali la 11 na 12 lakini alishindwa swali la 13, 14 na 15 kutoka shule inayotumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia. ............................................................................................................................ 75

Kielelezo Na. 27: Mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi swali la 11 na 12 lakini alishindwa swali la 13, 14 na 15 kutoka shule inayotumia Kiingereza kufundishia na kujifunzia. ....... 76

Kielelezo Na. 28: Mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi maswali yote matano. ..................... 80

Kielelezo Na. 29: Mwanafunzi kutoka shule inayotumia Lugha ya Kiswahili kufundishia aliyejibu kwa usahihi mafumbo yaliyohusu dhana ya kujumlisha katika swali la 16,18 na19 lakini alishindwa yaliyohusu dhana ya kutoa katika swali la 17 na 20. ............................ 81

Kielelezo Na. 30: Mwanafunzi kutoka shule inayotumia Kiingereza kufundishia aliyejibu kwa usahihi mafumbo yaliyohusu dhana ya kujumlisha katika swali la 16,18 na19 lakini alishindwa yaliyohusu dhana ya kutoa katika swali la 17 na 20. ...................................... 82

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania lilipewa jukumu la kuendesha upimaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa Darasa la Pili mwaka 2015. Lengo la kufanya upimaji kwa wanafunzi wa Darasa la Pili ni kubainisha uwezo na umahiri wa wanafunzi katika kumudu stadi za KKK kwa shule za msingi.

Baraza la Mitihani liliandaa zana za upimaji pamoja na dodoso katika stadi zote tatu ili kuendesha upimaji na baadaye kuchambua taarifa za matokeo ya upimaji huo. Shule 66 kutoka wilaya 22 za mikoa 11 zilihusishwa katika upimaji huu. Shule 3 zilichaguliwa kutoka kila wilaya ambazo zilijumuisha shule moja inayotumia lugha ya Kiingereza katika kufundishia na mbili zinazotumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia. Uteuzi wa shule moja ulizingatia mazingira ya vijijini na shule mbili zikiwa katika mazingira ya mjini.

Jumla ya wanafunzi 5,992 kati ya 7,018 waliosajiliwa, walifanya upimaji katika Stadi zote tatu za KKK. Majibu ya wanafunzi waliofanya upimaji yalisahihishwa na kuchambuliwa ili kubaini kiwango cha umahiri wa utendaji wa wanafunzi katika stadi husika.

Uchambuzi wa jumla wa viwango vya utendaji kwa wanafunzi waliofanya upimaji vinaonesha wanafunzi wengi (86.83%) walikuwa na utendaji mzuri katika stadi zote tatu. Wanafunzi walio wengi (89.87%) waliweza zaidi Stadi ya Kusoma kuliko stadi za Kuandika (88.33%) na Kuhesabu (82.28%). Aidha, katika Stadi ya Kuhesabu utendaji wa wanafunzi ni wa kiwango cha chini kuliko Stadi za Kusoma na Kuandika.

Baraza la Mitihani limeandaa taarifa hii ili kutoa mrejesho kwa wadau wa elimu hususan walimu wa shule kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK. Taarifa hii imegawanywa katika sura sita, Sura ya Kwanza ni Utangulizi, Sura ya Pili hadi ya Nne inaelezea Upimaji wa Stadi ya Kusoma, Kuandika na Kuhesabu, Sura ya Tano inaelezea Uchambuzi wa Madodoso na Sura ya Sita ni Maoni, Mapendekezo na Hitimisho.

Ni matumaini ya Baraza kuwa taarifa hii itakuwa chachu kwa wadau wote wa elimu katika kuweka msingi bora zaidi wa ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK na hivyo kuongeza umahiri wa wanafunzi katika kumudu stadi hizi kwa miaka ijayo.

Dr. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

# SURA YA KWANZA

## SAMPULI, ZANA ZA UPIMAJI NA UCHAMBUZI WA TAKWIMU

### 1.1 Utangulizi

Baraza la Mitihani liliendesha upimaji wa stadi za Kuhesabu na Kuandika tarehe 23/11/2015 na Upimaji wa stadi ya Kusoma tarehe 24/11/2015. Katika Upimaji huo vitendo vya Kusikiliza Sauti, Kutamka maneno, Kukokotoa na Kuandika vilifanyika ili kubaini umahiri wa wanafunzi hao katika stadi zote tatu. Sura hii inaelezea sampuli ya upimaji, zana zilizotumika kufanya upimaji na uchambuzi wa takwimu.

### 1.2 Sampuli ya Upimaji

Upimaji ulihusisha jumla ya shule 66 zilizoteuliwa kutoka katika mikoa 11 ambayo ni Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Pwani, Rukwa, Ruvuma na Shinyanga. Katika kila mkoa ziliteuliwa wilaya mbili na katika kila wilaya ziliteuliwa shule tatu. Uteuzi wa shule hizo ulizingatia vigezo vya ufaulu, mahali shule ilipo na lugha ya kufundishia. Shule 2 zilitumia lugha ya Kiswahili wakati shule 1 ilitumia lugha ya Kiingereza. Aidha, katika shule 3 zilizoteuliwa zilikuwepo za kijijini na mjini.

Jumla ya wanafunzi 7,018 kutoka halmashauri 22 zilizoteuliwa, walisajiliwa kushiriki katika upimaji. Kati ya wanafunzi hao, wanafunzi 5,992 sawa na asilimia 85.4 walishiriki katika upimaji. Wanafunzi wengine 1,026 sawa na

asilimia 14.6 hawakuweza kushiriki katika upimaji kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za utoro na ugonjwa.

## 1.3 Zana Zilizotumika Kufanya Upimaji

Maswali ya kupima stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu na madodoso yaliandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania (Rejea Kiambatanisho 1 – 13). Maswali ya upimaji yalilenga kupima viwango vya utendaji kwa kila mwanafunzi. Aidha, madodoso yalitayarishwa kwa ajili ya Walimu Wakuu, Wasimamizi Wakuu na Wasimamizi wa darasani kwa lengo la kukusanya taarifa ya hali ya kila kituo cha upimaji (shule) na mazingira yake ya kufundishia na kujifunzia kama vile, upatikanaji wa vitabu vya kufundishia na kujifunzia KKK na uwepo wa walimu waliopata mafunzo ya kufundisha KKK.

## 1.4 Uchambuzi wa Takwimu

Uchambuzi wa Takwimu ulifanyika kwa kila stadi zilizopimwa,ikiwa ni pamoja na kuzingatia mahali shule ilipo (mjini au vijijini) na lugha inayotumika kufundishia na kujifunzia. Uchambuzi uliofanyika katika stadi zote ulilenga kubaini umahiri wa kila mwanafunzi katika stadi husika. Umahiri huo ulipimwa katika skeli ya utendaji hafifu (0-12), wastani (13-25), mzuri (26-38) na mzuri sana (39-50).

Takwimu za umahiri uliobainika kwa watahiniwa zimefafanuliwa kwa kutumia majedwali na chati. Aidha, vielelezo kutoka kwenye skripti za wanafunzi vimetumika ili kuonesha majibu ya baadhi ya wanafunzi kwa kila swali kwa lengo la kuonesha namna walivyomudu au kushindwa

kumudu stadi husika. Kwa ujumla umahiri wa wanafunzi katika stadi zote tatu unaonekana kuwa mzuri. Jedwali Na. 1 linaonesha idadi ya wanafunzi waliofanya upimaji kwa kila stadi na walioweza kuwa na umahiri wa wastani hadi mzuri sana.

**Jedwali Na 1: Idadi ya Wanafunzi Waliofanya Upimaji na Kuonesha Utendaji wa Wastani hadi Mzuri Sana**

| Na. | Stadi | Waliofanya | Utendaji (Wastani hadi mzuri sana) | (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kusoma | 5,992 | 5,385 | 89.87 |
| 2. | Kuandika | 5,987 | 5,288 | 88.32 |
| 3. | Kuhesabu | 5,977 | 4,918 | 82.28 |

# SURA YA PILI

# UPIMAJI WA STADI YA KUSOMA

## 2.1 Utangulizi

Uchambuzi wa upimaji wa umahiri wa wanafunzi katika Stadi ya Kusoma ulifanyika kwa kila swali kwa kuzingatia vigezo vya utendaji. Aidha, ulinganifu wa umahiri katika utendaji wa wanafunzi ulifanyika kwa kuzingatia kigezo cha lugha wanayotumia kujifunza (Kiswahili/Kiingereza) na mahali (mjini/kijijini) ilipo shule anayosoma mwanafunzi. Sura hii inaeleza muundo wa karatasi ya upimaji katika Stadi ya Kusoma, vigezo vya utendaji wa mwanafunzi katika kumudu stadi hiyo na uchambuzi wa majibu ya mwanafunzi.

## 2.2 Muundo wa Karatasi ya Upimaji wa Kusoma

Upimaji wa Stadi ya Kusoma ulikuwa na karatasi moja ambayo ilikuwa imeandaliwa kwa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wanaotumia Kiswahili kama lugha ya kujifunzia na lugha ya Kiingereza kwa wanafunzi waliotumia lugha ya Kiingereza. Kila karatasi ya upimaji ilikuwa na maswali matatu. Swali la kwanza lilihusu kusoma maneno ishirini (20), swali la pili lilihusu kusoma sentensi tano (5) zenye jumla ya maneno ishirini (20) na swali la tatu lilikuwa la ufahamu ambapo mwanafunzi alitakiwa kusoma kifungu cha habari na kujibu maswali manne kwa mdomo.

Kazi ya upimaji kwa kila mwanafunzi ilitakiwa kukamilika kwa muda wa dakika kumi na tano (15). Dakika tano zilitumiwa na mwanafunzi kujibu maswali na dakika kumi (10) zilitumiwa na

msimamizi kwa ajili ya kukokotoa na kujaza alama za mwanafunzi katika skeli ya upimaji kwa maswali yote.

## 2.3 Vigezo vya Utendaji katika Stadi ya Kusoma

Viwango vya utendaji wa mwanafunzi katika upimaji wa stadi ya Kusoma viligawanywa katika makundi manne ambayo ni utendaji mzuri sana (maneno 16-20), mzuri (maneno 11-15), wastani (maneno 6-10) na hafifu (maneno 1-5) kwa kuzingatia idadi ya maneno aliyoweza kusoma kwa usahihi katika swali la kwanza na la pili. Aidha, katika swali la tatu viwango vya utendaji wa wanafunzi vilipimwa kwa kuzingatia idadi ya maswali ya ufahamu aliyoweza kujibu mwanafunzi kwa mdomo baada ya kusoma kifungu cha habari. Mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi maswali manne (4) utendaji wake ulikuwa mzuri sana, maswali matatu (3) utendaji mzuri, maswali mawili (2) utendaji wa wastani na swali moja ni utendaji hafifu.

## 2.4 Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi

### 2.4.1 Swali la 1: Kusoma Maneno

Swali la kwanza lilikuwa na maneno ishirini ambayo mwanafunzi alitakiwa kutumia dakika moja kuyasoma maneno yote kwa ufasaha. Idadi ya wanafunzi waliofanya swali hilo walikuwa ni 5,992.


Uchambuzi wa takwimu katika swali hili unaonesha kwamba umahiri wa wanafunzi ulikuwa mzuri sana kwani asilimia 90.2 ya wanafunzi waliweza kusoma maneno 6 hadi 20. Kati yao wanafunzi 4,870 sawa na

asilimia 81.28 waliweza kusoma kwa sauti na kwa ufasaha maneno 16 hadi 20 (utendaji mzuri sana) ambayo ni zaidi ya robo tatu ya maneno yote kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na 2: Utendaji wa Wanafunzi katika Kusoma Maneno**

| Maneno | Utendaji | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| **0 – 5** | Hafifu | 589 | 9.83 |
| **6 – 10** | Wastani | 195 | 3.25 |
| **11 – 15** | Mzuri | 338 | 5.64 |
| **16 – 20** | Mzuri Sana | 4,870 | 81.28 |
| | **Jumla** | 5,992 | 100.00 |

Wanafunzi 338 sawa na asilimia 5.64 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji walikuwa na utendaji mzuri kwa kuwa waliweza kusoma kwa sauti na kwa ufasaha maneno 11 hadi 15 ambayo ni zaidi ya nusu ya maneno yote kama inavyoonekana katika Kielelezo Na.1.



Weka alama ya **mkwaju** (/) kwa maneno yote ambayo mwanafunzi **ameshindwa** kuyasoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi aliposahihisha kusoma neno alilokuwa amekosea, zungushia (Ø) neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi **alama** 00¹/₂).


| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| jua | asubuhi | tano | simba | mchezo |
| wazazi | chungwa | shati | watu | weka |
| kimbia | panya | vitabu | siku | kijani |
| tisa | rubani | maji | asante | mguu |

Put a **stroke mark** (/) in all words which the pupil has failed to read and circle (Ø) self-correction if you already marked the word incorrect. (Each correct word is a 00¹/₂ **mark**).

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| sun | morning | five | lion | game |
| parents | orange | shirt | people | put |
| run | rat | books | day | green |
| nine | pilot | water | thanks | foot |

Kielelezo Na. 1: Majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno kumi na tano (15) kwa muda wa dakika moja.

Wanafunzi 195 sawa na asilimia 3.25 walikuwa na utendaji wa wastani kwa kuwa waliweza kusoma kwa sauti na kwa ufasaha maneno 6 hadi 10 ambayo ni chini ya nusu au nusu ya maneno yote kama inavyoonekana katika Kielelezo Na.2.



1. Kusoma maneno (alama 10).

Weka alama ya **mkwaju (/)** kwa maneno yote ambayo mwanafunzi **ameshindwa** kuyasoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi aliposahihisha kusoma neno alilokuwa amekosea, zungushia **(Ø)** neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi **alama** $00^1/_2$).

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| jua | asubuhi | tano | simba | mchezo |
| wazazi | chungwa | shati | watu | weka |
| kimbia | panya | vitabu | siku | kijani |
| tisa | rubani | maji | asante | mguu |

1. Reading of words (10 marks)


Put a **stroke mark (/)** in all words which the pupil has failed to read and circle **(Ø)** self-correction if you already marked the word incorrect. (Each correct word is a **$00^1/_2$ mark**).

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| sun | morning | five | lion | game |
| parents | orange | shirt | people | put |
| run | rat | books | day | green |
| nine | pilot | water | thanks | foot |

Kielelezo Na. 2: Majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno kumi (10) kwa muda wa dakika moja.

Pamoja na utendaji wa wastani, mzuri na mzuri sana wa wanafunzi 5,403 katika kusoma maneno, wanafunzi 589 sawa na asilimia 9.83 walikuwa na utendaji hafifu. Kati yao wanafunzi 173 sawa na asilimia 2.9 waliweza kusoma kwa usahihi neno 1 hadi maneno 5 ambayo ni chini ya robo au robo ya maneno yote kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 3.

Kielelezo Na. 3: Majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno matano (05) kwa muda wa dakika mbili



1. Kusoma maneno (alama 10).

Weka alama ya **mkwaju** (/) kwa maneno yote ambayo mwanafunzi **ameshindwa** kuyasoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi aliposahihisha kusoma neno alilokuwa amekosea, zungushia (Ø) neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi **alama 00$^{1}/_{2}$**).


| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| jua | asubuhi | tano | simba | mchezo |
| wazazi | chungwa | shati | watu | weka |
| kimbia | panya | vitabu | siku | kijani |
| tisa | rubani | maji | asante | mguu |

1. Reading of words (10 marks)

Put a **stroke mark** (/) in all words which the pupil has failed to read and circle (Ø) self-correction if you already marked the word incorrect. (Each correct word is a **00$^{1}/_{2}$ mark**).

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| sun | morning | five | lion | game |
| parents | orange | shirt | people | put |
| run | rat | books | day | green |
| nine | pilot | water | thanks | foot |

Aidha, wanafunzi 416 sawa na asilimia 6.9 walishindwa kabisa kusoma hata neno moja kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 4.



Weka alama ya **mkwaju** (/) kwa maneno yote ambayo mwanafunzi **ameshindwa** kuyasoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi aliposahihisha kusoma neno alilokuwa amekosea, zungushia (Ø) neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi **alama 00$^{1}/_{2}$**).

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| jua | asubuhi | tano | simba | mchezo |
| wazazi | chungwa | shati | watu | weka |
| kimbia | panya | vitabu | siku | kijani |
| tisa | rubani | maji | asante | mguu |

Put a **stroke mark** (/) in all words which the pupil has failed to read and circle (Ø) self-correction if you already marked the word incorrect. (Each correct word is a **00$^{1}/_{2}$ mark**).


| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| sun | morning | five | lion | game |
| parents | orange | shirt | people | put |
| run | rat | books | day | green |
| nine | pilot | water | thanks | foot |

Kielelezo Na. 4: Majibu ya wanafunzi walioshindwa kusoma hata neno moja.

#### 2.4.1.1 Wanafunzi Wanaojifunza kwa Lugha ya Kiswahili

Uchambuzi wa takwimu za utendaji wa wanafunzi katika swali la kwanza unaonesha kuwa zaidi ya asilimia 75 ya wanafunzi wanaojifunza kwa lugha ya Kiswahili walikuwa na umahiri wa kusoma maneno. Wanafunzi hao waliweza kusoma maneno yote ishirini (20) kwa ufasaha kama inavyoonekana katika Chati Na. 1.

**Chati Na. 1: Wanafunzi walioweza Kusoma Maneno**





Aidha, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wapo wanafunzi walioshindwa kusoma maneno yanayoundwa na herufi mwambatano ambayo ni

*asante, chungwa* na *panya* pamoja na neno *mguu* linaloundwa na silabi yenye konsonanti pekee. Wanafunzi hao hawakuwa na stadi za kusoma silabi zinazoundwa na konsonanti pekee au konsonanti mbili na irabu. Kwa upande mwingine, wanafunzi walishindwa kutamka kwa usahihi neno *rubani* kwani walitamka *lubani*. Utamkaji huu ulisababishwa na athari za lugha ya awali (lugha mama) ambapo sauti /r/ ilitamkwa /l/.

#### 2.4.1.2 Wanafunzi Wanaojifunza kwa Lugha ya Kiingereza

Upimaji wa wanafunzi wanaojifunza kwa lugha ya Kiingereza unaonesha kuwa, utendaji ulikuwa mzuri sana katika kusoma maneno. Hata hivyo, wapo wanafunzi walioshindwa kusoma kwa ufasaha baadhi ya maneno kama inavyoonekana katika Chati Na. 2.

**Chati Na. 2: Wanafunzi Walioshindwa Kusoma Maneno**




Chati Na. 2 inaonesha kuwa wanafunzi walishindwa zaidi kusoma maneno matatu ambayo ni *pilot* (25.86%), *thanks* (23.35%) na *people* (16.05%). Wanafunzi hao walishindwa kuhusisha umbo la neno *pilot* na neno *people* na matamshi yake kwa kuwa hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya umbo la maneno hayo na matamshi. Vilevile wanafunzi walishindwa kutamka neno '*thanks*' kwa sababu walichanganya sauti (th) /Ɵ/ na /s/.

### 2.4.2 Swali la 2: Kusoma Sentensi

Swali lilikuwa na sentensi tano (5) zilizoundwa na maneno manne kwa kila sentensi na hivyo kufanya jumla ya maneno ishirini (20) katika swali. Mwanafunzi alitakiwa kusoma kwa ufasaha sentensi zote kwa dakika moja.


Matokeo ya upimaji wa viwango vya utendaji yanaonesha kuwa asilimia 82.43 ya wanafunzi wote

waliweza kusoma kwa sauti na kwa ufasaha maneno 16 hadi 20 ambayo ni zaidi ya robo tatu ya maneno yote yaliyokuwa katika sentensi husika hivyo kuwa na utendaji mzuri sana kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 3.

**Jedwali Na 3: Utendaji wa Wanafunzi katika Kusoma Sentensi**

| Maneno | Utendaji | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| **0 – 5** | Hafifu | 596 | 9.94 |
| **6 – 10** | Wastani | 164 | 2.74 |
| **11 – 15** | Mzuri | 293 | 4.89 |
| **16 – 20** | Mzuri Sana | 4939 | 82.43 |
| | **Jumla** | 5992 | 100.00 |

Wanafunzi 293 sawa na asilimia 4.89 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji wa stadi ya kusoma walikuwa na utendaji mzuri kwa kuwa waliweza kusoma kwa sauti na kwa ufasaha maneno 11 hadi 15 kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 5.


Weka alama ya **mkwaju (/)** kwa maneno yote katika sentensi ambayo mwanafunzi **ameshindwa** kuyasoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi aliposahihisha kusoma neno alilokuwa amekosea, zungushia (Ø) neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi **alama 01**).

Magari ni mazuri sana.

Wazazi wangu ni wakarimu.

Mwalimu wetu ni mzuri.

Mimi nilifua nguo zangu.

Tanzania ni nchi yangu

Put a **stroke mark (/)** in all words in a sentence which the pupil has failed to read and circle **(Ø)** self-correction if you already marked the word in a sentence incorrect. (Each correct word in a sentence is a **01 mark**).

Cars are very nice.

My parents are kind.


Our teacher is good.

I washed my clothes.

Tanzania is my country.

Kielelezo Na. 5: Majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno 15 kwa dakika moja.


Wanafunzi 164 sawa na asilimia 2.74 walikuwa na utendaji wa wastani kwa kuwa waliweza kusoma kwa sauti na kwa ufasaha maneno 6 hadi 10 ambayo ni chini ya nusu au nusu ya maneno yote yaliyokuwa katika sentensi kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 6.



| Weka alama ya **mkwaju (/)** kwa maneno yote katika sentensi ambayo mwanafunzi **ameshindwa** kuyasoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi aliposahihisha kusoma neno alilokuwa amekosea, zungushia **(Ø)** neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi **alama 01**). | Put a **stroke mark (/)** in all words in a sentence which the pupil has failed to read and circle **(Ø)** self-correction if you already marked the word in a sentence incorrect. (Each correct word in a sentence is a **01 mark**). |
|---|---|
| Magari ni mazuri sana. | Cars are very nice. |
| Wazazi wangu ni wakarimu. | My parents are kind. |
| Mwalimu wetu ni mzuri. | Our teacher is good. |
| Mimi nilifua nguo zangu. | I washed my clothes. |
| Tanzania ni nchi yangu | Tanzania is my country. |

Kielelezo Na. 6: Majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno kumi kwa dakika moja.

Wanafunzi 596 sawa na asilimia 9.94 walikuwa na utendaji hafifu kwa kuwa waliweza kusoma kwa ufasaha neno 1 hadi maneno 5 ambayo ni chini ya robo au robo ya maneno yote yaliyokuwa katika sentensi kama yanavyoonekana katika Kielelezo Na. 7.



| Weka alama ya **mkwaju (/)** kwa maneno yote katika sentensi ambayo mwanafunzi **ameshindwa** kuyasoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi aliposahihisha kusoma neno alilokuwa amekosea, zungushia **(Ø)** neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi **alama 01**). | Put a **stroke mark (/)** in all words in a sentence which the pupil has failed to read and circle **(Ø)** self-correction if you already marked the word in a sentence incorrect. (Each correct word in a sentence is a **01 mark**). |
|---|---|
| Magari ni mazuri sana. | Cars are very nice. |
| Wazazi wangu ni wakarimu. | My parents are kind. |
| Mwalimu wetu ni mzuri. | Our teacher is good. |
| Mimi nilifua nguo zangu. | I washed my clothes. |
| Tanzania ni nchi yangu | Tanzania is my country. |

Kielelezo Na. 7: Majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno matano kwa dakika moja.

Aidha, baadhi ya wanafunzi walishindwa kabisa kusoma hata neno moja katika sentensi walizopewa kwa kuwa hawakuwa na stadi ya kusoma kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 8

| | |
|---|---|
| Weka alama ya **mkwaju (/)** kwa maneno yote katika sentensi ambayo mwanafunzi **ameshindwa** kuyasoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi aliposahihisha kusoma neno alilokuwa amekosea, zungushia **(Ø)** neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi **alama 01**). | Put a **stroke mark (/)** in all words in a sentence which the pupil has failed to read and circle **(Ø)** self-correction if you already marked the word in a sentence incorrect. (Each correct word in a sentence is a **01 mark**). |
| Magari ni mazuri sana. | Cars are very nice. |
| Wazazi wangu ni wakarimu. | My parents are kind. |
| Mwalimu wetu ni mzuri. | Our teacher is good. |
| Mimi nilifua nguo zangu. | I washed my clothes. |
| Tanzania ni nchi yangu | Tanzania is my country. |

Kielelezo Na. 8: Majibu ya wanafunzi walioshindwa kusoma hata neno moja.

### 2.4.2.1 Wanafunzi Wanaojifunza kwa Lugha ya Kiswahili

Uchambuzi uliofanyika katika usomaji wa sentensi unaonesha kuwa katika sentensi “magari ni mazuri sana” baadhi ya wanafunzi walishindwa kusoma neno '*mazuri*' (17.17%) na '*magari*' (16.66%) kwa sababu walikuwa wanachanganya sauti /r/ na /l/ katika kutamka silabi *–ri.*

Utendaji wa wanafunzi ulikuwa mzuri katika kusoma sentensi ya pili “Wazazi wangu ni wakarimu” ingawa asilimia 21.36 ya wanafunzi walishindwa kusoma neno

'*wakarimu'* kwa sababu walitamka sauti /l/ badala ya /r/. Vilevile asilimia 19.65 ya wanafunzi walishindwa kusoma neno "*wangu"* kwa sababu ya kuwepo kwa silabi "ngu" iliyoundwa na herufi mwambatano "ng".

Aidha, asilimia 20.55 ya wanafunzi walishindwa kusoma neno "*mwalimu"* katika sentensi ya tatu "Mwalimu wetu ni mzuri" kwa sababu neno hili limeundwa na herufi mwambatano "mw". Kwa upande mwingine, asilimia 19.01 ya wanafunzi walishindwa kusoma neno *"mzuri"* kwa kuwa walishindwa kutofautisha sauti /r/ na /l/ katika matamshi yao.


Utendaji wa wanafunzi katika sentensi "Mimi nilifua nguo zangu" unaonesha kuwa wanafunzi walioshindwa kusoma neno '*zangu'* walikuwa asilimia 18.37 na *nguo* asilimia 18.13. Wanafunzi hao walishindwa kusoma maneno hayo kwa kuwa yaliundwa na herufi mwambatano "ng".

Wanafunzi 1,316 sawa na asilimia 28.14 walishindwa kusoma neno '*nchi'* katika sentensi "Tanzania ni nchi yangu" ambalo limeundwa na silabi "n" na "chi" kwa sababu silabi "n" haina irabu na "chi" imeundwa na herufi mwambatano. Aidha, asilimia 21.34 ya wanafunzi walishindwa kusoma neno

“*Tanzania”* kwa sababu ya herufi mwambatano “nz”. Vilevile, neno *yangu* halikusomwa kwa usahihi na asilimia 20.23 ya wanafunzi kwa sababu liliundwa na herufi mwambatano “ng”.

Kwa ujumla wanafunzi walionesha umahiri mkubwa katika sentensi ya kwanza “Magari ni mazuri sana” iliyoundwa na maneno yenye silabi zilizotokana na konsonanti na irabu moja. Kwa upande mwingine sentensi ya tano “Tanzania ni nchi yangu” ilikuwa na idadi kubwa ya wanafunzi walioshindwa kusoma kwa usahihi maneno yote ikilinganishwa na sentensi zingine kwa sababu iliundwa na maneno matatu yenye herufi mwambatano. Pia, wanafunzi walikosa umahiri wa kutosha katika maneno yaliyoundwa na silabi zenye herufi “r” na “l” kama inavyoonekana katika Chati Na. 3.


**Chati Na. 3: Utendaji wa Wanafunzi katika Usomaji wa Sentensi**




### 2.4.2.2 Wanafunzi Wanaojifunza kwa lugha ya Kiingereza

Uchambuzi wa takwimu za utendaji wa wanafunzi katika swali la pili unaonesha kuwa, wanafunzi walikuwa na umahiri wa kusoma sentensi. Wanafunzi hao walikuwa na utendaji mzuri sana katika sentensi ya kwanza, tatu na nne, na utendaji mzuri katika sentensi ya pili na tano. Chati Na. 4 inaonesha viwango vya utendaji wa wanafunzi katika kila sentensi.

**Chati Na. 4: Asilimia ya Wanafunzi katika Usomaji wa Sentensi**




Pamoja na utendaji wa wanafunzi kuwa mzuri katika usomaji wa sentensi, asilimia 36.12 ya wanafunzi walishindwa kusoma neno '*kind*' katika sentensi “My parents are kind” kwa sababu matamshi ya neno hilo hayana uhusiano wa moja kwa moja na umbo la neno.

### 2.4.3 Swali la 3: Ufahamu

Swali la tatu lilihusu ufahamu ambapo wanafunzi walitakiwa kusoma kifungu cha habari na kujibu maswali manne kwa mdomo kwa muda wa dakika tatu. Kifungu cha habari kwa wanafunzi wanaofundishwa na kujifunza kwa lugha ya Kiswahili kilikuwa kama ifuatavyo:

> Baraka na Tumaini ni marafiki, wanaishi kijiji cha Mtakuja. Watoto hawa wanasoma katika shule ya msingi Mtakuja. Wote wako darasa la pili. Walimu wao wanawapenda sana, kwa sababu wana akili. Katika matokeo ya muhula uliopita, Tumaini alikuwa wa kwanza. Rafiki yake alikuwa wa pili darasani kwao. Wote wawili walifurahi sana. Katika sherehe ya kufunga shule, wote wawili walipewa zawadi nzuri.

Aidha kifungu cha habari kwa wanafunzi wanaofundishwa na kujifunza kwa lugha ya Kiingereza kilikuwa kama ifuatavyo:

> Baraka and Tumaini are friends. They are in standard two at Mtakuja primary school. Their teachers' like them because they are clever. In the last term test results, Tumaini was the first. His friend was the second in their class. They were happy. At the end of the year, there was a party. In that party they were given nice gifts.

Umahiri wa wanafunzi katika swali la tatu ulikuwa chini kidogo ikilinganishwa na umahiri katika swali la kwanza na la pili. Hata hivyo, asilimia 78.05 ya wanafunzi waliweza kujibu kwa usahihi maswali mawili (2) hadi manne (4). Miongoni mwao asilimia 25.23 ya wanafunzi walikuwa na utendaji mzuri sana kwa kuwa walijibu maswali yote manne kwa usahihi kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 9:

**Maswali na Majibu**

Endapo mwanafunzi atatoa jibu sahihi, zungushia alama **5** na iwapo mwanafunzi atatoa jibu lisilo sahihi zungushia alama **0** na kisha andika jumla ya alama kwenye jedwali lifuatalo:

| Na. | Maswali na Majibu | alama | |
|---|---|---|---|
| (a) | Rafiki yake Tumaini anaitwa nani? **(Baraka)** | ⑤ | 0 |
| (b) | Baraka na Tumaini wanasoma darasa gani? **(Darasa la Pili)** | ⑤ | 0 |
| (c) | Nani alikuwa wa kwanza katika matokeo ya muhula uliopita? **(Tumaini)** | ⑤ | 0 |
| (d) | Kwa nini walimu wanawapenda Baraka na Tumaini? **(kwa sababu wana akili)** | ⑤ | 0 |
| | **Jumla** | 20 | |

**Questions and Answers**

If the pupil will give a correct answer, circle 5 marks and if he/she will give incorrect answer, circle 0 mark and then write a total marks in the space provided in the table.

| No. | Questions and Answers | Marks | |
|---|---|---|---|
| (a) | Who is Tumaini's friend? **(Baraka)** | ⑤ | 0 |
| (b) | In what class is Baraka and Tumaini? **(Standard two)** | ⑤ | 0 |
| (c) | Who was the first one in the last term results? **(Tumaini)** | ⑤ | 0 |
| (d) | Why do teachers like Baraka and Tumaini?. **(Because they were clever)** | ⑤ | 0 |
| | **Total** | 20 | |

Kielelezo Na. 9: Majibu ya wanafunzi walioweza kusoma habari na kujibu maswali yote manne kwa usahihi.

Wanafunzi 1,849 sawa na asilimia 30.86 walikuwa na utendaji mzuri kwa kuwa waliweza kujibu kwa usahihi maswali matatu (3) ambayo ni robo tatu ya maswali waliyoulizwa kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 10.

**Maswali na Majibu**

Endapo mwanafunzi atatoa jibu sahihi, zungushia alama **5** na iwapo mwanafunzi atatoa jibu lisilo sahihi zungushia alama **0** na kisha andika jumla ya alama kwenye jedwali lifuatalo:

| Na. | Maswali na Majibu | alama | |
|---|---|---|---|
| (a) | Rafiki yake Tumaini anaitwa nani? **(Baraka)** | ⑤ | 0 |
| (b) | Baraka na Tumaini wanasoma darasa gani? **(Darasa la Pili)** | ⑤ | 0 |
| (c) | Nani alikuwa wa kwanza katika matokeo ya muhula uliopita? **(Tumaini)** | ⑤ | 0 |
| (d) | Kwa nini walimu wanawapenda Baraka na Tumaini? **(kwa sababu wana akili)** | 5 | ⓪ |
| | **Jumla** | 15 | |

**Questions and Answers**

If the pupil will give a correct answer, circle 5 marks and if he/she will give incorrect answer, circle 0 mark and then write a total marks in the space provided in the table.

| No. | Questions and Answers | Marks | |
|---|---|---|---|
| (a) | Who is Tumaini's friend? **(Baraka)** | ⑤ | 0 |
| (b) | In what class is Baraka and Tumaini? **(Standard two)** | ⑤ | 0 |
| (c) | Who was the first one in the last term results? **(Tumaini)** | ⑤ | 0 |
| (d) | Why do teachers like Baraka and Tumaini?. **(Because they were clever)** | 5 | ⓪ |
| | **Total** | 15 | |

Kielelezo Na. 10: Majibu ya wanafunzi walioweza kujibu maswali matatu ya ufahamu

Wanafunzi 1,316 sawa na asilimia 21.96 walikuwa na utendaji wa wastani kwa kuwa waliweza kujibu maswali mawili (2) ambayo ni nusu ya maswali waliyopewa kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 11.

**Maswali na Majibu**

Endapo mwanafunzi atatoa jibu sahihi, zungushia alama **5** na iwapo mwanafunzi atatoa jibu lisilo sahihi zungushia alama **0** na kisha andika jumla ya alama kwenye jedwali lifuatalo:

| Na. | Maswali na Majibu | alama | |
|---|---|---|---|
| (a) | Rafiki yake Tumaini anaitwa nani? **(Baraka)** | 5 | (0) |
| (b) | Baraka na Tumaini wanasoma darasa gani? **(Darasa la Pili)** | (5) | 0 |
| (c) | Nani alikuwa wa kwanza katika matokeo ya muhula uliopita? **(Tumaini)** | (5) | 0 |
| (d) | Kwa nini walimu wanawapenda Baraka na Tumaini? **(kwa sababu wana akili)** | 5 | (0) |
| | **Jumla** | 10 | |

**Questions and Answers**

If the pupil will give a correct answer, circle 5 marks and if he/she will give incorrect answer, circle 0 mark and then write a total marks in the space provided in the table.

| No. | Questions and Answers | Marks | |
|---|---|---|---|
| (a) | Who is Tumaini's friend? **(Baraka)** | (5) | 0 |
| (b) | In what class is Baraka and Tumaini? **(Standard two)** | (5) | 0 |
| (c) | Who was the first one in the last term results? **(Tumaini)** | 5 | (0) |
| (d) | Why do teachers like Baraka and Tumaini?. **(Because they were clever)** | 5 | (0) |
| | **Total** | 10 | |

Kielelezo Na. 11: Majibu ya wanafunzi walioweza kujibu maswali mawili ya ufahamu.

Wanafunzi 694 sawa na asilimia 11.06 walikuwa na utendaji hafifu kwa kuwa waliweza kujibu swali moja tu (1) ambalo ni robo ya maswali waliyoulizwa. Wanafunzi hao walitumia muda mrefu kusoma kwa sababu walikuwa wanasoma kwa kusitasita na hivyo kushindwa kukumbuka maudhui yaliyomo katika kifungu cha habari. Kielelezo Na. 12 kinaonesha utendaji hafifu wa wanafunzi katika upimaji.

**Maswali na Majibu**

Endapo mwanafunzi atatoa jibu sahihi, zungushia alama **5** na iwapo mwanafunzi atatoa jibu lisilo sahihi zungushia alama **0** na kisha andika jumla ya alama kwenye jedwali lifuatalo:

| Na. | Maswali na Majibu | alama | |
|---|---|---|---|
| (a) | Rafiki yake Tumaini anaitwa nani?<br>**(Baraka)** | 5 | ⓪ |
| (b) | Baraka na Tumaini wanasoma darasa gani?<br>**(Darasa la Pili)** | ⑤ | 0 |
| (c) | Nani alikuwa wa kwanza katika matokeo ya muhula uliopita?<br>**(Tumaini)** | 5 | ⓪ |
| (d) | Kwa nini walimu wanawapenda Baraka na Tumaini?<br>**(kwa sababu wana akili)** | 5 | ⓪ |
| | Jumla | 5 | |

**Questions and Answers**

If the pupil will give a correct answer, circle 5 marks and if he/she will give incorrect answer, circle 0 mark and then write a total marks in the space provided in the table.

| No. | Questions and Answers | Marks | |
|---|---|---|---|
| (a) | Who is Tumaini's friend?<br>**(Baraka)** | ⑤ | 0 |
| (b) | In what class is Baraka and Tumaini?<br>**(Standard two)** | 5 | ⓪ |
| (c) | Who was the first one in the last term results?<br>**(Tumaini)** | 5 | ⓪ |
| (d) | Why do teachers like Baraka and Tumaini?.<br>**(Because they were clever)** | 5 | ⓪ |
| | Total | 5 | |

Kielelezo Na. 12: Utendaji wa wanafunzi walioweza kujibu swali moja la Ufahamu.

Aidha, wanafunzi 618 sawa na asilimia 10.3 walishindwa kujibu maswali yote yaliyopima ufahamu kwa sababu walishindwa kusoma kifungu cha habari walichopewa. Kielelezo Na. 13 kinaonesha sampuli ya majibu ya baadhi ya wanafunzi walioshindwa kujibu maswali yote kutoka katika kifungu cha habari alichotakiwa kusoma.

**Maswali na Majibu**

Endapo mwanafunzi atatoa jibu sahihi, zungushia alama **5** na iwapo mwanafunzi atatoa jibu lisilo sahihi zungushia alama **0** na kisha andika jumla ya alama kwenye jedwali lifuatalo:

| Na. | Maswali na Majibu | alama | |
|---|---|---|---|
| (a) | Rafiki yake Tumaini anaitwa nani? **(Baraka)** | 5 | 0 |
| (b) | Baraka na Tumaini wanasoma darasa gani? **(Darasa la Pili)** | 5 | 0 |
| (c) | Nani alikuwa wa kwanza katika matokeo ya muhula uliopita? **(Tumaini)** | 5 | 0 |
| (d) | Kwa nini walimu wanawapenda Baraka na Tumaini? **(kwa sababu wana akili)** | 5 | 0 |
| | **Jumla** | 0 | |

**Questions and Answers**

If the pupil will give a correct answer, circle 5 marks and if he/she will give incorrect answer, circle 0 mark and then write a total marks in the space provided in the table.

| No. | Questions and Answers | Marks | |
|---|---|---|---|
| (a) | Who is Tumaini's friend? **(Baraka)** | 5 | 0 |
| (b) | In what class is Baraka and Tumaini? **(Standard two)** | 5 | 0 |
| (c) | Who was the first one in the last term results? **(Tumaini)** | 5 | 0 |
| (d) | Why do teachers like Baraka and Tumaini?. **(Because they were clever)** | 5 | 0 |
| | **Total** | 0 | |

Kielelezo Na. 13: Majibu ya wanafunzi walioshindwa kujibu maswali yote ya Ufahamu.

#### 2.4.3.1 Wanafunzi Wanaotumia Lugha ya Kiswahili kujifunzia

Umahiri wa wanafunzi katika swali la tatu ulikuwa mzuri kwani takwimu zinaonesha asilimia 75.83 ya wanafunzi waliweza kujibu maswali mawili au zaidi waliyoulizwa kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 4.

**Jedwali Na 4: Utendaji wa Wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiswahili katika Kujibu Maswali ya Ufahamu**

| Idadi ya Maswali | Viwango vya Utendaji | Idadi ya Wanafunzi | Asilimia ya Wanafunzi |
|---|---|---|---|
| **1** | Hafifu | 1,130 | 24.16 |
| **2** | Wastani | 1,046 | 22.36 |
| **3** | Mzuri | 1,406 | 30.06 |
| **4** | Mzuri sana | 1,095 | 23.41 |
| | **Jumla** | **4,677** | **100.00** |

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, kati ya maswali manne ya ufahamu waliyoulizwa wanafunzi, swali la nne “Kwa nini walimu wanampenda Baraka na Tumaini” halikujibiwa vizuri na baadhi ya wanafunzi kwa sababu walitakiwa kufanya tathmini.

Katika swali la tatu wanafunzi walionesha umahiri wa kiwango cha chini ukilinganisha na swali la kwanza na la pili katika upimaji huu. Sababu zilizochangia hali hiyo ni pamoja na wanafunzi kutokuwa na umahiri katika stadi ya kusoma kifungu cha habari, kusoma bila kuwa na umakini wa kuelewa kile walichokisoma na hivyo kukosa kumbukumbu, kusoma neno moja moja na hivyo kushindwa kuunganisha sentensi ili kupata maana ya alichokisoma.

#### 2.4.3.2 Wanafunzi wanaojifunza kwa Lugha ya Kiingereza

Wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiingereza kujifunzia walionesha umahiri wa kiwango cha juu katika swali la tatu kwani asilimia 85.93 ya wanafunzi wote waliweza kujibu kwa usahihi maswali mawili na zaidi ya ufahamu waliyoulizwa kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 5.

**Jedwali Na 5: Utendaji wa Wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiingereza katika Kujibu Maswali ya Ufahamu.**

| Idadi ya Maswali | Viwango vya Utendaji | Idadi ya Wanafunzi | Asilimia ya Wanafunzi |
|---|---|---|---|
| **1** | Hafifu | 185 | 14.07 |
| **2** | Wastani | 270 | 20.53 |
| **3** | Mzuri | 443 | 33.69 |
| **4** | Mzuri sana | 417 | 31.71 |
| | **Jumla** | **1,315** | **100.00** |

Aidha, kati ya maswali manne ya ufahamu waliyoulizwa wanafunzi, wengi wao walishindwa kujibu swali la nne kwa sababu walitakiwa kutoa tathmini. Jambo hili lililojitokeza hata kwa wanafunzi wanaosoma kwa lugha ya Kiswahili.

Pamoja na utendaji wa wanafunzi katika swali la tatu kuwa mzuri sana, utendaji huo ulikuwa wa chini ukilinganishwa na utendaji wa wanafunzi katika swali la 1 na 2 kwa sababu baadhi ya wanafunzi hawakuweza kusoma kabisa kifungu cha habari. Wanafunzi wengine walikuwa wakisoma kwa kusitasita na hivyo kutumia muda mrefu katika kusoma kifungu cha habari, hali ambayo iliwasababishia kusahau kile walichokisoma awali. Aidha, wapo wanafunzi waliokuwa wanasoma bila kuwa na umahiri wa ufahamu/kuelewa katika kile walichokuwa


wanakisoma. Sababu hizi ziliwafanya wanafunzi washindwe kujibu kabisa au washindwe kujibu kwa usahihi maswali waliyoulizwa.

## 2.5 Ulinganifu wa Umahiri Kishule na Lugha ya Kufundishia

### 2.5.1 Umahiri wa Wanafunzi kwa Shule za Mjini na Vijijini

Jumla ya shule 23 za mjini na 43 za vijijini zilitumika katika kufanya upimaji wa umahiri wa wanafunzi wa Darasa la Pili katika stadi ya Kusoma. Matokeo ya utendaji wa wanafunzi katika stadi ya kusoma kwa kuzingatia mahali (mjini/vijijini) yanaonesha kuwa umahiri wa wanafunzi katika shule za mjini ulikuwa mzuri zaidi kwa asilimia 5.56 kwani umahiri wa shule hizo ulikuwa asilimia 93.15 wakati ule wa shule za vijijini ulikuwa asilimia 87.59 kama inavyoonekana katika chati Na. 5.


**Chati Na. 5: Umahiri wa wanafunzi wa Shule za Mjini na Vijijini katika Upimaji wa Stadi ya Kusoma**




### 2.5.2 Ulinganifu wa Umahiri kwa Wanafunzi Waliofanya Upimaji kwa Lugha ya Kiswahili na Kiingereza

Jumla ya wanafunzi waliofanya upimaji katika stadi ya Kusoma walikuwa 5,992, kati yao 4,677 wanatumia lugha ya Kiswahili kujifunzia na 1,315 wanatumia lugha ya Kiingereza. Matokeo ya upimaji yanaonesha kuwa wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiingereza walikuwa na utendaji mzuri sana ambapo asilimia 99.16 ya wanafunzi walikuwa na viwango vya utendaji kati ya mzuri sana, mzuri na wastani ikilinganishwa na wanaojifunza kwa kutumia lugha ya kiswahili ambapo asilimia 87.26 ya wanafunzi walikuwa na viwango vya utendaji kati ya mzuri sana, mzuri na wastani. Chati Na.6. inaonesha viwango vya utendaji kulingana na lugha ya kujifunzia.

**Chati Na. 6: Umahiri wa Wanafunzi wanaotumia Lugha ya Kingereza na Kiswahili**




Aidha, umahiri wa wanafunzi wa shule za vijijini zinazotumia lugha ya Kiingereza kujifunzia ulikuwa ni mzuri zaidi kwa asilimia 13.23 ikilinganishwa na wanafunzi wa shule za vijijini wanaotumia lugha ya Kiswahili kujifunzia ambapo umahiri wao ulikuwa asilimia 85.3. Vilevile, wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiingereza kujifunzia waliopo katika shule za mjini walikuwa na umahiri mzuri zaidi kwa asilimia 9.21 ambapo umahiri wao ulikuwa asilimia 99.72 wakati umahiri wa wanaotumia lugha ya Kiswahili ulikuwa asilimia 90.51.

### 2.5.3 Muhtasari wa Uchambuzi katika Stadi ya Kusoma

Kwa ujumla wanafunzi walikuwa na umahiri mzuri katika kusoma kwa ufasaha maneno, sentensi na kifungu cha habari pamoja na kujibu maswali kwa

usahihi. Wanafunzi wachache ambao hawakufanya vizuri, hawakuwa na umahiri wa kusoma maneno yenye herufi mwambatano katika swali la kwanza na la pili, vilevile hawakuwa na umahiri wa kusoma kwa ufasaha kifungu cha habari na hivyo kushindwa kujibu maswali ya ufahamu.

# SURA YA TATU

# UPIMAJI WA STADI YA KUANDIKA

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza muundo wa karatasi ya upimaji, vigezo vya utendaji wa wanafunzi katika kumudu Stadi ya Kuandika na uchambuzi wa majibu ya wanafunzi. Uchambuzi wa upimaji wa Stadi ya Kuandika pamoja na majibu ya wanafunzi ulifanyika katika kila swali kwa kuzingatia vigezo vya utendaji. Ulinganifu wa umahiri katika utendaji wa wanafunzi ulifanyika kwa kuzingatia shule zinazotumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia na zile zinazotumia lugha ya Kiingereza katika kufundishia.

Aidha, ulinganifu wa umahiri wa wanafunzi ulifanyika kwa kuzingatia maeneo ya shule zilipo (mijini/vijijini). Viwango vya Utendaji vya wanafunzi vya jumla katika Stadi ya Kuandika viligawanyika katika makundi manne. Makundi hayo yalikuwa utendaji hafifu ikiwa mwanafunzi alipata alama 0 hadi 12, utendaji wa wastani alama 13 hadi 25, utendaji mzuri alama 26 hadi 38, na utendaji mzuri sana alama 39 hadi 50.

## 3.2 Muundo wa Karatasi ya Upimaji wa Kuandika

Karatasi ya Upimaji wa Stadi ya Kuandika ilikuwa na maswali matatu. Swali la kwanza ni la imla na lilikuwa na vipengele kumi. Swali la pili liliwataka wanafunzi kuandika maneno kwa herufi kubwa ambalo lilikuwa na vipengele kumi. Swali la tatu lilikuwa la kunakili kifungu cha maneno ambacho kilitakiwa kukamilishwa kwa kuwekwa alama za uandishi. Lugha

zilizotumika katika Upimaji wa Stadi ya Kuandika zilikuwa Kiswahili kwa shule zinazotumia lugha ya Kiswahili katika kufundisha na kujifunza na Kiingereza kwa shule zinazotumia lugha ya Kiingereza katika kufundisha na kujifunza.

## 3.3 Vigezo vya Utendaji katika Stadi ya Kuandika kwa kila Swali

Viwango vya umahiri wa mwanafunzi katika Kuandika uligawanywa katika makundi manne ambapo katika swali la 1 na la 2 mwanafunzi aliyeweza kuandika neno 1 hadi maneno 2 alipata utendaji hafifu, maneno 3 hadi 5 ulikuwa utendaji wa wastani, maneno 6 hadi maneno 8 utendaji mzuri na aliyeweza kuandika maneno 9 hadi maneno 10 kwa usahihi alikuwa na utendaji mzuri sana. Katika swali la 3 mwanafunzi aliyeweza kuweka alama ya uandishi na kuweza kunakili kwa usahihi maneno 3 alipata utendaji hafifu, maneno 8 na alama 2 utendaji wa wastani, maneno 13 na alama 3 utendaji mzuri na mwanafunzi aliyeweza kunakili maneno 15 na kuweka alama zote za uandishi kwa usahihi alikuwa na utendaji mzuri sana.

## 3.4 Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi


### 3.4.1 Swali la 1: Imla

Swali hili lilikuwa na jumla ya maneno kumi ambapo mwalimu alitakiwa kusoma kila neno kwa sauti na kwa umakini mara mbili. Mwanafunzi alitakiwa aandike neno lililosomwa kwa herufi ndogo. Mwalimu alisoma tena maneno yote kwa mara ya mwisho ili mwanafunzi afanye marekebisho kwa maneno aliyokosea. Swali

lilikuwa na jumla ya alama 20 ambapo kila neno lilikuwa na alama 2.

Utendaji wa jumla katika swali la 1 unaonesha kuwa wanafunzi 726 sawa na asilimia 12.13 walishindwa kuandika neno lolote au waliweza kuandika kwa usahihi neno 1 hadi maneno 2 ambao ni utendaji hafifu. Wanafunzi 568 sawa na asilimia 9.49 waliweza kuandika maneno 3 hadi 5 ambapo walikuwa na utendaji wa wastani. Aidha, wanafunzi 1,372 sawa na asilimia 22.92 waliweza kuandika kwa usahihi maneno 6 hadi 8 ambao ni Utendaji mzuri. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi 3,321 sawa na asilimia 55 waliweza kuandika maneno 9 hadi 10 ambapo ni utendaji mzuri sana. Kwa ujumla umahiri wa wanafunzi katika swali hili ni asilimia 78.39 ambao ni utendaji mzuri. Chati Na. 7 inaonesha muhtasari wa utendaji wa wanafunzi katika swali la 1.

**Chati Na. 7: Utendaji wa Wanafunzi katika Uandishi wa Imla**




Maneno yaliyotumika katika Upimaji wa Kuandika Imla yalifanyiwa uchambuzi wa kina kama ifuatavyo:

**(a) ndege/bird**

Uchambuzi unaonesha kuwa jumla ya wanafunzi 3,396 wanaotoka katika shule zinazotumia lugha ya Kiswahili kufundishia ambao ni sawa na asilimia 73 waliweza kuandika neno “ndege” kwa usahihi. Hii inaonesha kuwa wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha katika kuhusisha sauti na herufi mwambatano "nd". Aidha, uchambuzi umebaini kuwa jumla ya wanafunzi 1,281 sawa na asilimia 27.39 walishindwa kuandika neno “ndege” kwa usahihi. Sababu zilizofanya wanafunzi hao washindwe kuandika kwa usahihi neno “ndege’ ni kushindwa kuhusisha sauti na herufi mwambatano "nd". Kwa mfano, badala ya mwanafunzi kuandika neno “ndege” aliandika “*dege”* na mwanafunzi mwingine aliandika “*deke”.*

Uchambuzi uliofanywa kwa wanafunzi wanaosoma kwa kutumia lugha ya Kiingereza unaonesha kuwa, wanafunzi 771 sawa na asilimia 58.85 walishindwa kuandika kwa usahihi neno "bird". Wanafunzi hao walikosa uwezo wa kuhusisha sauti ambapo wakati wa kutamka neno "bird" konsonanti "r" humezwa na haisikiki wakati wa kutamkwa na wengine waliandika neno "bed" badala ya "bird" kutokana na matamshi sawa ya maneno hayo.

**(b) shoka/axe**

Jumla ya wanafunzi 3,619 kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiswahili kufundishia ambao ni sawa na asilimia 77.38 waliweza kuandika neno "shoka" kwa usahihi. Uchambuzi zaidi umebaini kuwa jumla ya wanafunzi 1,058 sawa na asilimia 22.62 walishindwa kuandika neno "shoka" kwa usahihi. Wanafunzi walioshindwa kuandika neno "shoka" kwa usahihi walikosa umahiri na uwezo wa kuhusisha sauti na herufi mwambatano "sh" wakati wa kuandika neno "shoka". Kwa mfano, badala ya kuandika neno "shoka" baadhi ya wanafunzi waliandika "hoka". Hii inadhihirisha kuwa wanafunzi hao walishindwa kuandika herufi mwambatano "sh".

Aidha, wanafunzi 850 wanaosoma katika shule zinazofundisha kwa lugha ya Kiingereza, ambao ni sawa na asilimia 64.89 waliweza kuandika neno "axe" kwa usahihi. Wanafunzi hao walionesha umahiri wa kubaini sauti moja katika lugha ya Kiingereza

inayoumbwa na neno lenye herufi tatu. Hali kadhalika jumla ya wanafunzi 460 sawa na asilimia 35.11 walikosa umahiri wa namna ya kuandika herufi za neno "axe". Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi waliandika "Asi" badala ya "axe".

**(c) nzi/fly**

Takwimu katika uandishi wa neno “nzi” zimeonesha kuwa jumla ya wanafunzi 2,692 wanaosoma kwa kutumia lugha ya Kiswahili sawa na asilimia 57.56 waliweza kuandika kwa usahihi neno "nzi". Wanafunzi hao walionesha kuwa na uwezo wa kuhusisha sauti ya silabi yenye herufi mwambatano "nz". Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi hao hawakuathiriwa na matamshi ya mazoea ya kila siku yaani "inzi" na waliweza kubaini sauti zinazomezwa wakati wa kutamka neno "nzi".

Takwimu za uchambuzi zinaonesha kuwa jumla ya wanafunzi 1,985 sawa na asilimia 42.44 walishindwa kuandika neno "nzi" kwa usahihi. Wanafunzi hao walishindwa kuandika neno hilo kutokana na kushindwa kuhusisha sauti za herufi mwambatano "nz" ikiwa ni pamoja na kushindwa kubaini tofauti iliyopo baina ya matamshi na namna ya kuandika neno "nzi".

Wanafunzi 1,007 sawa na asilimia 76.87 wanaosoma katika shule zinazofundisha kwa kutumia lugha ya Kiingereza waliweza kujibu swali hili kwa usahihi.

Wanafunzi hao waliweza kuandika neno "fly" kwa usahihi kwa kuwa neno hili linaandikwa kama linavyotamkwa hivyo ilikuwa rahisi kuhusisha sauti na kinachoandikwa.

Takwimu zinabainisha zaidi kuwa wanafunzi 303 sawa na asilimia 23.13 walishindwa kuandika neno "fly" kwa usahihi. Hii inadhihirisha kuwa wanafunzi hao walishindwa kuhusisha sauti za herufi mwambatano tatu ambazo ni konsonanti zinazounda neno "fly". Pia athari ya matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiingereza kujifunzia ilijidhihirisha kwa baadhi ya wanafunzi ambapo waliandika neno la Kiingereza "fly" kwa Kiswahili. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi waliandika "flay" badala ya “fly”.

**(d) saa/watch**

Uchambuzi wa takwimu za utendaji unaonesha kuwa jumla ya wanafunzi 3,930 wanaojifunza kwa kutumia lugha ya Kiswahili sawa na asilimia 84.03 waliweza kuandika neno “saa” kwa usahihi. Hii inaonesha kuwa wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kubaini silabi zinazoundwa na irabu kama vile “a” katika neno "saa".

Jumla ya wanafunzi 747 ambao ni sawa na asilimia 15.97 walishindwa kuandika neno “saa” kwa sababu walishindwa kutambua silabi zinazoundwa na irabu peke yake na hivyo kuandika "sa" badala ya "saa". Sababu nyingine ni mwingiliano wa lugha mama na maneno ya Kiswahili. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi waliandika neno "zaa" badala ya "saa".

Uchambuzi zaidi umebaini kuwa jumla ya wanafunzi 1,310 kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia wamelijibu swali hili ambapo kati yao wanafunzi 703 sawa na asilimia 53.66 waliweza kuandika neno 'watch' kwa usahihi. Wanafunzi hao walionesha kuwa na umahiri wa kuhusisha sauti za konsonanti mwambatano "watch" ambazo hutamkwa kama silabi moja katika lugha ya Kiingereza.

Hata hivyo, jumla ya wanafunzi 607 sawa na asilimia 46.33 walishindwa kuandika kwa usahihi neno "watch" kwani hawakuweza kukumbuka tahjia ya neno "watch" na kuandika maneno kama *woch*, *wach* na *warch*.

**(e) taa/lamp**

Jumla ya wanafunzi 3,869 wanaotumia lugha ya Kiswahili kujifunzia sawa na asilimia 82.72 waliweza kuandika neno "taa" kwa usahihi. Wanafunzi hao walionesha kuwa na umahiri wa kutosha katika kuhusisha sauti na silabi zinazoundwa na irabu bila konsonanti.

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa jumla ya wanafunzi 808 sawa na asilimia 17.28 walishindwa kujibu kipengele hiki kwa usahihi. Wanafunzi hao waliandika "ta" badala ya kuandika neno "taa". Sababu zilizowafanya wanafunzi hao kushindwa kuandika neno "taa" kwa usahihi ni kutokana na kushindwa kubaini mkazo wa sauti uliopo katika irabu mbili zilizofuatana wakati wa kutamka neno "taa".

Wanafunzi 879 sawa na asilimia 67 wanaotoka shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia waliweza kujibu swali hili vizuri kwa kuandika neno "lamp" kwa usahihi. Wanafunzi hao waliweza kuandika neno "lamp" kwa usahihi kwa sababu matamshi/ sauti ya neno hilo haitofautiani na jinsi linavyoandikwa.

Aidha, jumla ya wanafunzi 431 ambao ni sawa na asilimia 33 walishindwa kuandika neno “lamp” kwa usahihi. Wanafunzi hao walikosa umahiri wa kuhusisha sauti na namna ya kuandika neno "lamp". Aidha, baadhi ya wanafunzi hao waliandika neno "lap" na "lamb" kwa kukosea kutokana na kushindwa kuhusisha sauti na uumbaji wa herufi za neno hilo.

**(f) viatu/shoes**

Jumla ya wanafunzi 3,630 sawa na asilimia 77.61 kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiswahili kufundishia waliweza kuandika neno “viatu” kwa usahihi. Wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kuhusisha sauti na silabi zinazounda neno “viatu”. Aidha, muundo wa silabi zinazounda neno “viatu” ni rahisi na ni muundo wa moja kwa moja jambo lililosababisha wanafunzi kuweza kuandika neno “viatu” kwa usahihi.

Hata hivyo, jumla ya wanafunzi 1,047 sawa na asilimia 22.39 walishindwa kuandika neno “viatu” kwa usahihi. Wanafunzi hao walishindwa kuhusisha sauti na silabi zinazounda neno “viatu”. Aidha, athari ya lugha mama

miongoni mwa wanafunzi hao, kulisababisha washindwe kuandika neno “viatu”. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi waliandika, "nziatu" na wengine “fiatu” badala ya “viatu”.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa jumla ya wanafunzi 904 sawa na asilimia 69 kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia waliweza kuandika neno "*shoes*" kwa usahihi kwa kuwa walikuwa na uelewa wa kuhusisha sauti ya neno "shoes" na uumbaji wa herufi za konsonanti mbili "sh" zinazoumba neno "shoes".

Aidha, takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi 406 sawa na asilimia 31 walishindwa kuandika neno "shoes" kwa usahihi. Baadhi ya wanafunzi waliweza kuandika herufi za konsonanti “sh” lakini wakashindwa kukamilisha neno “shoes” kwa usahihi. Kwa mfano, waliandika maneno kama "sheos"  "*shose*", "*shuse*", "*shoaze*" na "*shourse*" ambayo siyo maneno sahihi ya lugha ya Kiingereza. Hivyo wanafunzi hao hawakuwa na ujuzi mpana wa tahjia za maneno mbalimbali ya Kiingereza.

**(g) chumba/room**

Jumla ya wanafunzi 3,525 sawa na asilimia 75.37 kutoka shule zinazofundisha kwa kutumia lugha ya Kiswahili waliweza kuandika neno 'chumba' kwa usahihi. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa wa

kuhusisha sauti zinazounda herufi mwambatano "ch" na irabu "u" katika silabi "chu" na "mba" hivyo kuweza kuandika neno chumba kwa urahisi.

Uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 1,152 sawa na asilimia 24.63 walishindwa kujibu swali hili kwani hawakuweza kuandika neno “chumba” kwa usahihi. Wanafunzi hao walishindwa kuhusisha sauti za herufi za konsonanti "ch" na irabu "u" hivyo, badala ya kuandika neno “chumba” waliandika maneno mengine yasiyo na maana katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi waliandika neno “humba". Aidha, athari ya lugha mama ilisababisha baadhi ya wanafunzi kutoweza kuandika neno “chumba” kwa usahihi, kuongeza maneno ya kilugha mwanzoni mwa neno “chumba”. Kwa mfano, wapo wanafunzi walioandika "jichumba".

Uchambuzi zaidi wa takwimu za utendaji wa wanafunzi wanaotoka shule zinazofundisha kwa lugha ya Kiingereza unaonesha kuwa, jumla ya wanafunzi 1,086 sawa na asilimia 83 waliojibu swali hili waliweza kuandika neno "room" kwa usahihi. Wanafunzi hao walionesha kuwa na umahiri wa kutambua sauti ya irabu mfuatano "oo" ambazo katika lugha ya Kiingereza hutamkwa kwa sauti moja. Wanafunzi walioshindwa kuandika neno 'room' waliandika maneno kama '*rum* '*rom*' na '*loom*'.

**(h) gauni/dress**

Jumla ya wanafunzi 3,680 sawa na asilimia 78.68 kutoka shule zinazofundisha kwa lugha ya Kiswahili waliweza kuandika neno “gauni” kwa usahihi. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa wa kutosha wa kubaini sauti zinazoumbwa kwa muunganiko wa silabi bila kuingiliwa na herufi mwambatano.

Hata hivyo, wanafunzi 997 sawa na asilimia 21.32 walishindwa kuandika neno “gauni” kwa usahihi kwa kuwa walishindwa kuhusisha sauti ya herufi zinazounda neno “gauni” na kuandika maneno yasiyo sahihi kama "gu" na "gau". Aidha, baadhi ya wanafunzi waliweza kuandika neno “gauni” kwa usahihi, lakini waliathiriwa na lugha mama jambo lililosababisha waongeze maneno ya kilugha mwanzoni mwa neno “gauni”. Kwa mfano baadhi ya wanafunzi waliandika "ngauni" na "hekigauni”.

Kwa upande wa wanafunzi wanaotoka shule zinazofundisha kwa lugha ya Kiingereza, wanafunzi 846 sawa na asilimia 64.58 walijibu kipengele hiki kwa usahihi kwani waliweza kuandika neno "dress". Wanafunzi hao waliweza kuhusisha sauti na umbo la herufi mbili za konsonanti “ss” ambazo katika lugha ya Kiingereza hutamkwa kwa pamoja.

Uchambuzi zaidi umebaini kuwa wanafunzi 464 sawa na asilimia 35.42 walishindwa kuandika kwa usahihi neno "dress" kwa sababu hawakuweza kutambua tahjia ya neno "dress" na badala yake waliandika herufi ambazo haziundi maneno ya lugha ya

Kiingereza. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi waliandika "drus", "drees" na "dres" kimakosa badala ya kuandika neno sahihi "dress".

**(i) nyeusi/black**

Jumla ya wanafunzi 3,461 sawa na asilimia 74 kutoka shule zinazofundisha kwa lugha ya Kiswahili waliweza kujibu kipengele hiki vizuri. Wanafunzi hao walionesha kuwa na uelewa wa kutosha wa kuhusisha sauti ya herufi mwambatano zinazounda silabi "nye" wakati wa kuandika neno “nyeusi”.

Uchambuzi zaidi wa takwimu za umahiri wa wanafunzi umebaini kuwa wanafunzi 1,216 sawa na asilimia 26 walishindwa kuandika neno “nyeusi” kwa usahihi kutokana na kukosa umahiri wa kubaini sauti na herufi mwambatano katika silabi "nye" katika kuandika neno “nyeusi”. Baadhi ya wanafunzi waliandika "heusi" na "usis" ambayo siyo maneno katika lugha ya Kiswahili. Wanafunzi walipaswa kuandika kilichosomwa tu.


Takwimu za uchambuzi wa umahiri wa wanafunzi kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia unaonesha kuwa, wanafunzi 1,160 sawa na asilimia 89 waliweza kujibu kipengele hiki kwa kuandika neno "black" kwa usahihi. Aidha, walionesha kuwa na uelewa wa kutosha katika kubaini sauti inayoumbwa na konsonanti mbili yaani "ck" na kuwafanya waweze kuandika neno "black" kwa usahihi. Wanafunzi walioshindwa kuandika neno "black" kwa usahihi waliandika "*blak*", "*blank*" "dlock" na "*brack*".

**(j) meza/table**

Kipengele hiki kilijibiwa kwa usahihi na jumla ya wanafunzi 3,797 sawa na asilimia 81.18 kutoka shule zinazofundisha kwa lugha ya Kiswahili. Sababu zilizowafanya wanafunzi hao kuweza kuandika neno “meza” kwa usahihi ni kuwa na ujuzi wa kutosha wa kubaini silabi mbili zinazounda neno “meza”.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, wanafunzi 1,133 sawa na asilimia 87 waliweza kujibu swali hili kwa kuandika neno "table" kwa usahihi. Wanafunzi wanaosoma katika shule zinazotumia lugha ya Kiingereza wameonesha kuwa na umahiri wa kutosha wa kuhusisha sauti ya silabi mbili na umbo la neno "table". Wanafunzi walioshindwa kuandika neno "table" kwa usahihi waliandika maneno kama "teba", "tabo" na "teble".

Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioandika kwa usahihi na walioshindwa kuandika kwa usahihi maneno katika kipengele (a) hadi (j) yameoneshwa katika Kielelezo Na. 14 na Na.15.




1. **Sikiliza** kwa makini maneno yanayosomwa na mwalimu kisha **andika maneno hayo kwa usahihi** katika nafasi zilizo wazi :

(a) Ndege
(b) Shoka
(c) NZi
(d) Saa
(e) Taa
(f) Viatu
(g) Chumba
(h) Gauni
(i) Nyeusi
(j) Meza

1. **Listen carefully** to the words being read by the teacher and then **write** those words correctly in the spaces provided:

(a) bird
(b) axe
(c) fly
(d) watch
(e) lamp
(f) shoes
(g) room
(h) dress
(i) black
(j) table

Kielelezo Na. 14: Sampuli ya majibu ya wanafunzi wanaosoma katika shule zinazotumia Kiswahili/Kiingereza katika kufundishia walioweza kuandika maneno kumi kwa usahihi.



1. Sikiliza kwa makini maneno yanayosomwa na mwalimu kisha andika maneno hayo kwa usahihi katika nafasi zilizo wazi :

(a) ______
(b) ndenge
(c) hoka
(d) sa
(e) ta
(f) vihafu
(g) chuba
(h) nyeusi
(i) gau
(j) meza


1. Listen carefully to the words being read by the teacher and then write those words correctly in the spaces provided:

(a) bed
(b) dcs
(c) clay
(d) woch
(e) bam
(f) shs
(g) room
(h) dres
(i) dlock
(j) tcbo

Kielelezo Na 15: Sampuli ya majibu ya wanafunzi wanaotumia Kiswahili/ Kiingereza kujifunzia walioweza kuandika maneno mawili ya Kiswahili na moja tu la Kiingereza kwa usahihi kati ya kumi.

Aidha, Chati Na. 8 inaonesha ulinganifu wa umahiri wa wanafunzi walioshindwa kuandika maneno kumi ya imla kwa kutumia lugha ya Kiswahili au Kiingereza.

**Chati Na. 8: Wanafunzi Walioshindwa Kuandika Maneno kwa Lugha ya Kiswahili na Kingereza**





| | Ndege / Bird | Shoka/ Axe | Nzi/ Fly | Saa/ Watch | Taa/ Lamp | Viatu/ Shoes | Chumba/ Room | Gauni/ Dress | Nyeusi / Black | Meza/ Table |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kiswahili (%) | 27.39 | 22.62 | 42.44 | 15.97 | 17.28 | 22.39 | 24.63 | 21.32 | 26.00 | 18.82 |
| Kiingereza (%) | 58.85 | 35.11 | 23.13 | 46.34 | 32.9 | 30.99 | 17.1 | 35.42 | 11.45 | 13.51 |

Chati Na. 8 inaonesha kuwa wanafunzi waliowengi wanaotumia kiingereza kujifunzia walishindwa kuandika maneno ya Imla.

### 3.4.2 Swali la 2: Kutumia Herufi Kubwa kwa Usahihi katika Kuunda Maneno

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 5,987 kati ya wanafunzi 6,328 waliofanya upimaji huu. Jumla ya wanafunzi 950 sawa na asilimia 15.87 waliweza kuandika maneno 9 hadi 10 kwa herufi kubwa kwa usahihi na kupata alama 9 hadi 10 hivyo kuwa na utendaji mzuri sana. Wanafunzi hao waliweza kuandika kwa herufi kubwa na kuweza kuumba silabi za herufi mwambatano ilivyotakiwa. Kwa mfano, wanafunzi hao waliweza kuandika maneno kama "NYEUSI", "MLANGO", “CHUPA”, “NYUMBA”, “DHAHABU” na “SHINDWA” yenye herufi mwambatano kwa usahihi. Aidha, katika maneno ya

Kiingereza wanafunzi waliweza kuandika vizuri sana maneno kama “BLACK”, ‘BOTTLE” na “SPOON”. Kielelezo Na.16 kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi waliojibu vizuri kwa lugha ya Kiswahili na kwa lugha ya Kiingereza na kupata alama 10.


2. Andika maneno yafuatayo kwa herufi kubwa katika nafasi iliyo wazi.

(a) ua UA
(b) nyeusi NYEUSI
(c) mmea MMEA
(d) kijiko KIJIKO
(e) gari GARI
(f) mlango MLANGO
(g) chupa CHUPA
(h) nyumba NYUMBA
(i) dhahabu DHAHABU
(j) shindwa SHINDWA


2. Write the following words in capital letters in the spaces provided.

(a) flower FLOWER
(b) black BLACK
(c) plant PLANT
(d) spoon SPOON
(e) car CAR
(f) door DOOR
(g) bottle BOTTLE
(h) house HOUSE
(i) gold GOLD
(j) fail FAIL

Kielelezo Na. 16: Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kubadilisha maneno yaliyoandikwa kwa herufi ndogo kwa kuyaandika kwa herufi kubwa kwa usahihi.

Aidha, uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa baadhi ya wanafunzi (2,845) ambao ni sawa na asilimia 47.52 walishindwa kabisa kuandika maneno waliyopewa kwa herufi kubwa na baadhi waliweza kuandika neno moja au maneno mawili kwa usahihi kati ya maneno 10 waliyopewa. Utendaji wa wanafunzi hao ulikuwa ni hafifu kwani walipata alama 0 hadi 2. Baadhi ya wanafunzi walichanganya herufi kubwa na

ndogo wakati swali liliwataka kuandika kwa herufi kubwa tu. Kwa mfano, maneno waliyochanganya ni kama “shiNDWA”, “DHAhaBU”, “chuPA”, “kiJIKO”, “BLAck”, “DooR” “GoLD” na “FloWER”. Wengine waliandika maneno yote kwa herufi ndogo hivyo kushindwa kutofautisha kati ya herufi kubwa na ndogo. Vielelezo 17 na 18 vinaonesha sampuli za majibu ya wanafunzi waliokuwa na utendaji hafifu kwa kupata alama 0 hadi 2.


2. **Andika** maneno yafuatayo kwa **herufi kubwa** katika nafasi iliyo wazi.

(a) ua Ua

(b) nyeusi nYEUSI

(c) mmea mmEA

(d) kijiko KijiKO

(e) gari GAri

(f) mlango mLanGo

(g) chupa CHUpA

(h) nyumba nyumBA

(i) dhahabu DHAhAbU

(j) shindwa SHinDWA

Kielelezo Na. 17: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeandika maneno kwa kuchanganya herufi kubwa na ndogo.

2. **Write** the following words in **capital letters** in the spaces provided.

(a) flower flowers

(b) black black s

(c) plant plants

(d) spoon spoons

(e) car cars

(f) door door

(g) bottle bottle

(h) house houses

(i) gold gold

(j) fail fail

Kielelezo Na. 18: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeandika maneno yote kumi kwa herufi ndogo badala ya herufi kubwa. Aidha, mwanafunzi huyo katika baadhi ya maneno aliandika umbo "S" linaloonesha dhana ya wingi, jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya swali.

Aidha, wanafunzi 1,179 ambao ni sawa na asilimia 19.69 walikuwa na utendaji wa wastani kwa kuweza kuandika kwa herufi kubwa maneno 3 hadi 5 kwa usahihi. Sababu zilizowafanya wanafunzi hao kupata utendaji wa wastani ni pamoja na kuchanganya herufi kubwa na ndogo kwa baadhi ya maneno, jambo linaloonesha kuwa wanafunzi hao walikosa umahiri wa kutofautisha herufi kubwa na ndogo.


Uchambuzi zaidi uliofanywa katika majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa asilimia 16.92 ambayo ni sawa na wanafunzi 1,013 waliweza kuandika maneno 6 hadi 8 na kuwa na utendaji mzuri. Sababu zilizochangia wanafunzi hao kufanya vizuri zilitokana na umahiri wao katika kuumba herufi kubwa. Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi hao walishindwa kuandika maneno kama "SHINDWA", "CHUPA" na "DHAHABU" ambayo yana silabi zenye herufi mwambatano. Kwenye shule zinazofundisha kwa lugha ya Kiingereza, wanafunzi walichanganya herufi kubwa na ndogo, kwa mfano waliandika "FLoWER", "GoLD", "DooR" na "SPooN," jambo linaloonesha kuwa hawakuwa na umahiri wa kuumba herufi O,U na L kubwa.

### 3.4.3 Swali la 3: Kunakili Kifungu cha Maneno na Kuweka Alama za Uandishi

Swali lilimtaka mwanafunzi kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi ambazo ni nukta (.), mkato (,), alama ya mshangao (!) na alama ya kuuliza (?). Swali lilikuwa na alama 20 zilizotokana na kunakili kwa usahihi maneno 15 na kuweka kwa usahihi alama 5 za uandishi.

Jumla ya wanafunzi waliofanya swali hili ni 5,983 ambao ni asilimia 94.5 ya wanafunzi wote waliosajiliwa kufanya upimaji huu. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa swali lilijibiwa vizuri ambapo asilimia

78.36 ya wanafunzi walipata utendaji mzuri kwa kupata alama 11 hadi 20. Hii inaonesha kuwa wanafunzi walikuwa na uelewa na umahiri mkubwa kuhusu stadi mahsusi ya kunakili kifungu cha maneno na matumizi ya alama za uandishi. Kielelezo Na. 19 kinaonesha mifano ya majibu ya wanafunzi walionakili kifungu cha maneno kwa usahihi na kuweka alama stahiki.


3. Copy the following paragraph and then put full stop (.): comma (,): exclamation mark (!) and question mark (?) correctly.

What did Furaha buy yesterday_____ She bought mangoes ____ oranges and bananas_____ Oh_____ they were sweet_____

What did Furaha buy yesterday? She bought mangoes, oranges and bananas. Oh! they were Sweet.

3. Nakili kifungu cha maneno kifuatacho na weka alama za nukta (.): mkato (,): alama ya kushangaa (!) na alama ya kuuliza (?) kwa usahihi.

Furaha alinunua nini sokoni jana____ Alinunua maembe____machungwa na ndizi____ Oh___ yalikuwa matunda matamu sana____


Furaha alinunua nini sokoni jana ? Alinunua maembe, machungwa na ndizi. Oh ! Yalikuwa matunda matamu sana.

Kielelezo Na. 19: Sampuli ya majibu ya wanafunzi walionakili kifungu cha maneno na kutumia alama za uandishi kwa usahihi.

Wanafunzi waliopata utendaji hafifu walikuwa 1,306 ambao ni sawa na asilimia 21.81. Wanafunzi hao walishindwa kuelewa matakwa ya swali hivyo kushindwa kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi. Aidha, wapo wanafunzi walionakili maelekezo ya swali badala ya kunakili kifungu cha habari. Wanafunzi walioshindwa kunakili kifungu cha

؟


maneno na kuweka alama za uandishi hawakuwa na umahiri katika stadi mahsusi ya kunakili kifungu cha maneno na matumizi ya alama za uandishi hivyo hawakuelewa matakwa ya swali. Kielelezo Na. 20 kinaonesha mfano wa majibu ambayo sio sahihi.



3. **Nakili** kifungu cha maneno kifuatacho na weka alama za **nukta (.): mkato (,): alama ya kushangaa (!)** na **alama ya kuuliza (?)** kwa usahihi.

Furaha alinunua nini sokoni jana______ Alinunua maembe______machungwa na ndizi______ Oh______ yalikuwa matunda matamu sana______

Kielelezo Na. 20: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweka alama za uandishi katika nafasi iliyoachwa wazi bila ya kunakili kifungu cha maneno. Aidha, baadhi ya alama aliziandika kwa kugeuza kwa mfano alama ya kuuliza ? iligeuzwa na kuandikwa na alama ya mkato, iligeuzwa na kuandikwa **c**.


3. Nakili kifungu cha maneno kifuatacho na weka alama za nukta (.): mkato (,): alama ya kushangaa (!) na alama ya kuuliza (?) kwa usahihi.

Furaha alinunua nini sokoni jana____ Alinunua maembe____machungwa na ndizi____ Oh____ yalikuwa matunda matamu sana____

3. Copy the following paragraph and then put full stop (.): comma (,): exclamation mark (!) and question mark (?) correctly.

What did Furaha buy yesterday____ She bought mangoes ____ oranges and bananas____ Oh____ they were sweet____

Kielelezo Na. 21: Sampuli za majibu ya wanafunzi walioweka alama katika kifungu cha maneno bila kunakili. Aidha, wanafunzi hao hawakuweka alama hizo kwa usahihi.

## 3.5 Ulinganifu wa Umahiri Kishule na Lugha ya Kufundishia

### 3.5.1 Umahiri kulingana na Lugha ya Kufundishia katika swali la 1

Uchambuzi wa takwimu za shule zinazotumia lugha ya Kiswahili kufundishia unaonesha kuwa jumla ya wanafunzi 599 ambao ni sawa na asilimia 12.81 waliweza kuandika kwa usahihi neno 1 hadi 2 au kushindwa kabisa kuandika maneno kumi waliyopewa na kupata alama 0 hadi 4 ambazo zinaonesha utendaji hafifu katika swali la 1.

Jumla ya wanafunzi 352 sawa na asilimia 7.53 waliweza kuandika kwa usahihi maneno 3 hadi 5 kati

ya maneno kumi waliyopewa na kupata alama 6 hadi 10 ambazo zinaonesha utendaji wa wastani.

Aidha, jumla ya wanafunzi 903 ambao ni sawa na asilimia 19.31 waliweza kuandika kwa usahihi maneno 6 hadi 8 kati ya maneno kumi waliyopewa na kupata alama 12 hadi 16 ambazo zinaonesha utendaji mzuri.

Uchambuzi zaidi wa utendaji wa wanafunzi unaonesha kuwa jumla ya wanafunzi 2,823 ambao ni sawa na asilimia 60.36 waliweza kuandika kwa usahihi maneno 9 hadi 10 kati ya maneno yote waliyopewa na kupata alama 18 hadi 20 ambazo zinaonesha utendaji mzuri sana.

Kwa upande wa shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia uchambuzi unaonesha kuwa, jumla ya wanafunzi 1,310 walijibu swali la 1. Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi 127 sawa na asilimia 9.69 waliweza kuandika kwa usahihi neno 1 hadi 2 au kushindwa kabisa kuandika neno lolote kati ya maneno kumi waliyopewa na kupata alama 0 hadi 4 ambazo zinaonesha utendaji hafifu.


Takwimu zaidi zinaonesha kuwa jumla ya wanafunzi 216 sawa na asilimia 16.47 waliweza kuandika kwa usahihi maneno 3 hadi 5 kati ya maneno kumi waliyopewa na kupata alama 6 hadi 10 ambazo zinaonesha utendaji wa wastani.

Aidha, wanafunzi 469 sawa na asilimia 35.8 waliweza kuandika kwa usahihi maneno 6 hadi 8 kati ya maneno

kumi waliyopewa na kupata alama 12 hadi 16 ambazo zinaonesha utendaji mzuri.

Jumla ya wanafunzi 498 sawa na asilimia 38.02 waliweza kuandika kwa usahihi maneno 9 hadi 10 kati ya maneno kumi waliyopewa na kupata alama 18 hadi 20 ambazo zinaonesha utendaji mzuri sana. Chati Na. 9 inatoa ufafanuzi wa ulinganifu wa umahiri wa wanafunzi kwa asilimia kwa kuzingatia kigezo cha lugha iliyotumika kufundishia.

**Chati Na. 9: Ulinganifu wa Umahiri wa Wanafunzi Wanaotumia Lugha ya Kiswahili na Kiingereza Kujifunzia katika Kuandika Imla.**




Uchambuzi wa takwimu katika Chati Na.9 unaonesha kuwa yapo maeneo machache ambayo shule zinazofundisha kwa kutumia lugha ya Kiingereza waliandika vizuri maneno ya imla. Hata hivyo, shule

zinazofundisha kwa kutumia lugha ya Kiswahili zimeonesha kuwa na utendaji mzuri sana katika kuandika maneno ya imla ikilinganishwa na shule zinazofundisha kwa kutumia lugha ya Kiingereza.

### 3.5.2 Ulinganifu wa Umahiri kwa Lugha ya Kufundishia katika Swali la 2


Wanafunzi 4,677 sawa na asilimia 78.12 kati ya wanafunzi 5,987 waliofanya upimaji wa Kuandika maneno kwa herufi kubwa, walijibu swali hili kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Aidha, wanafunzi 1,310 ambao ni sawa na asilimia 21.88 walijibu kwa kutumia lugha ya Kiingereza. Wanafunzi 361 sawa na asilimia 7.72 tu ndio walioweza kuandika maneno 9 hadi 10 kwa usahihi kwa kutumia lugha ya Kiswahili hivyo kuonesha utendaji mzuri sana. Wanafunzi 589 kati ya wanafunzi 1,310 sawa na asilimia 44.96 wanaosoma katika shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia walipata utendaji mzuri sana kwani waliweza kuandika maneno 9 hadi 10 kwa usahihi.

Ulinganifu wa takwimu za utendaji wa wanafunzi kwa kuzingatia lugha hizi mbili ulionesha kuwa wanafunzi 629 ambao ni sawa na asilimia 13.45 wanaotumia lugha ya Kiswahili na wanafunzi 384 sawa na asilimia 29.31 waliotumia lugha ya Kiingereza waliweza kuandika maneno 6 hadi 8 kwa herufi kubwa kwa usahihi na kupata alama 6 hadi 8 na hivyo kuonesha utendaji mzuri.

Utendaji wa wastani ulioneshwa na wanafunzi 985 wanaotumia lugha ya Kiswahili ambao ni sawa na asilimia 21.06 ambapo wanafunzi 194 wanaotumia lugha ya Kiingereza sawa na asilimia 14.81 waliweza kuandika maneno 3 hadi 5 kwa usahihi na kupata alama 3 hadi 5, hivyo kuonesha utendaji wa wastani.

Ulinganifu zaidi uliofanywa kwa kigezo cha lugha inayotumika kufundishia (Kiswahili au Kiingereza) ulibainisha kuwa utendaji hafifu umeoneshwa na wanafunzi 2,702 ambao wanatumia lugha ya Kiswahili kujifunzia sawa na asilimia 57.77 ambapo wanafunzi 143 tu wanaotumia lugha ya Kiingereza kujifunzia sawa na asilimia 10.92 ndio walionesha utendaji hafifu. Chati Na. 10 inaonesha ulinganifu wa utendaji kati ya wanafunzi wanaotoka shule zinazotumia lugha ya Kiswahili na wale wanaotoka shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia.

**Chati Na. 10: Ulinganifu wa Umahiri wa Wanafunzi katika Kuandika Herufi Kubwa kwa Kuzingatia Lugha ya Kufundishia**



Kwa ujumla, uchambuzi wa takwimu katika Chati Na.10 unaonesha kuwa wanafunzi wanaosoma katika shule zinazofundisha kwa kutumia lugha ya Kiingereza walifanya vizuri zaidi katika kubadili maneno yaliyoandikwa kwa herufi ndogo na kuyaandika kwa herufi kubwa kuliko wanafunzi wanaosoma katika shule zinazofundisha kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

### 3.5.3 Ulinganifu wa Umahiri kwa Lugha ya Kufundishia katika Swali la 3

Takwimu za matokeo zinaonesha kuwa swali la tatu lilijibiwa na wanafunzi 4,677 wanaosoma katika shule zinazofundisha kwa kutumia lugha ya Kiswahili kujifunzia. Wanafunzi hao walikuwa na utendaji mzuri sana kwani walipata alama kuanzia 11 hadi 16 sawa na asilimia 43.30. Wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiingereza kujifunzia walikuwa 1,310 sawa na asilimia 38.47 na walikuwa na utendaji mzuri. Wanafunzi wanaosoma kwa kutumia lugha ya Kiswahili waliopata utendaji hafifu kuanzia alama 0 hadi 4 walikuwa asilimia 25.44 wakati wanaotumia lugha ya Kiingereza walikuwa asilimia 8.85. Wanafunzi waliopata utendaji wa wastani na kupata alama 6 hadi 10 kwa wanaotumia lugha ya Kiswahili walikuwa asilimia 9.94 wakati wanaotumia lugha ya Kiingereza walikuwa asilimia 7.10. Wanafunzi waliopata utendaji mzuri sana kuanzia alama 17 hadi 20 wanaotumia lugha ya Kiswahili walikuwa asilimia 21.32 wakati wanaotumia lugha ya Kiingereza walikuwa asilimia 45.57.

Uchambuzi huu wa takwimu umeainishwa katika Jedwali Na. 6.

**Jedwali Na 6: Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Kunakili Kifungu cha Maneno na Kuweka Alama za Uandishi.**

| | Viwango vya Utendaji | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Lugha** | **Utendaji Hafifu** | **Utendaji wa Wastani** | **Utendaji Mzuri** | **Utendaji Mzuri Sana** |
| **Kiswahili** | 25.44 | 9.94 | 43.3 | 21.32 |
| **Kingereza** | 8.85 | 7.1 | 38.47 | 45.57 |

### 3.5.4 Ulinganifu wa Umahiri wa Stadi ya Kuandika kwa Kuzingatia Lugha ya Kufundishia na Maeneo Shule Zilipo

Kwa ujumla, wanafunzi 5,987 walifanya upimaji katika Stadi ya Kuandika. Utendaji wa jumla unaonesha kuwa wanafunzi 699 ambao ni sawa na asilimia 11.68 walikuwa na utendaji hafifu. Aidha, wanafunzi 5,288 ambao ni sawa na asilimia 88.33 walikuwa na utendaji wa Wastani, Mzuri na Mzuri Sana.

Utendaji wa jumla kwa kuzingatia lugha ya kufundishia unaonesha kuwa wanafunzi 661 ambao ni sawa na asilimia 14.13 wanaotoka shule zinazofundisha kwa kutumia lugha ya Kiswahili walikuwa na utendaji hafifu. Hata hivyo, wanafunzi 4,016 ambao ni sawa na

asilimia 85.86 walikuwa na utendaji wa wastani, mzuri na mzuri sana.


Jumla ya wanafunzi 34 ambao ni sawa na asilimia 2.9 wanaojifunza kwa kutumia lugha ya Kiingereza walikuwa na utendaji hafifu. Aidha, wanafunzi 1,272 ambao ni sawa na asilimia 97.09 walikuwa na utendaji wa wastani, mzuri na mzuri sana. Hivyo, uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi wanaojifunza kwa kutumia lugha ya Kiingereza walikuwa na utendaji mzuri zaidi ukilinganisha na wanafunzi wanaojifunza kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

Uchambuzi wa takwimu katika stadi ya Kuandika kwa kufanya ulinganifu zaidi katika majibu ya wanafunzi wa shule za vijijini na mjini unaonesha kuwa wanafunzi wanaosoma katika shule za mjini walifanya vizuri zaidi kuliko shule za vijijini.

Uchambuzi zaidi wa takwimu unaonesha kuwa wanafunzi 615 kutoka katika shule zilizopo kijijini na ambazo zinatumia lugha ya Kiingereza kufundishia walikuwa na utendaji hafifu ambao ulikuwa ni asilimia 2.6. Aidha, wanafunzi 1,845 sawa na asilimia 97.4 walikuwa na utendaji wa wastani, mzuri na mzuri sana. Kwa upande wa shule zinazotumia lugha ya Kiswahili kufundishia wanafunzi 495 sawa na asilimia 16.8 walikuwa na utendaji hafifu. Wanafunzi 2,451 ambao ni sawa na asilimia 83.2 walikuwa na utendaji wa wastani, mzuri na mzuri sana.

Aidha, kwa upande wa shule zilizopo katika maeneo ya mjini, uchambuzi wa takwimu umebainisha kuwa wanafunzi 695 sawa na asilimia 3.1 wanaotumia lugha ya Kiingereza kujifunzia walikuwa na utendaji hafifu. Hata hivyo, wanafunzi 2,085 sawa na asilimia 96.82 walikuwa na utendaji wa wastani, mzuri na mzuri sana. Kwa upande wa shule zinazotumia lugha ya Kiswahili kufundishia, jumla ya wanafunzi 169 sawa na asilimia 9.76 walikuwa na utendaji hafifu. Aidha, wanafunzi 1,562 ambao ni sawa na asilimia 90.24 walikuwa na utendaji wa wastani, mzuri na mzuri sana. Ufafanuzi zaidi kuhusu ulinganifu wa utendaji katika Stadi ya Kuandika kwa kuzingatia lugha ya kufundishia na maeneo shule zilipo umeoneshwa kwenye Chati Na. 11.

**Chati Na. 11: Ulinganifu wa Umahiri wa Wanafunzi katika Stadi ya Kuandika kwa Kuzingatia Lugha ya Kufundishia na Maeneo Shule Ilipo**



Mchanganuo wa takwimu za utendaji wa wanafunzi ulioainishwa katika Chati Na. 11 unabainisha kuwa utendaji wa wanafunzi ulitofautiana kutokana na lugha ya kufundishia na maeneo shule hizo zilipo. Uchambuzi wa takwimu umebainisha kwamba shule zilizopo mjini zilikuwa na utendaji mzuri zaidi (93.53%) katika stadi ya Kuandika zikilinganishwa na shule zilizopo vijijini ambazo zilikuwa na utendaji wa asilimia 90.3.

### 3.5.5 Muhtasari wa Uchambuzi katika Stadi ya Kuandika

Kwa ujumla, umahiri wa wanafunzi katika stadi ya kuandika ulikuwa mzuri. Hata hivyo, wanafunzi wengi wameonesha umahiri mkubwa sana katika kuandika maneno ya Imla ikilinganishwa na umahiri walionesha katika kuandika maneno kwa herufi kubwa, kunakili kifungu cha habari na kuweka alama za uandishi.

# SURA YA NNE

# UPIMAJI WA STADI YA KUHESABU

## 4.1 Utangulizi

Uchambuzi wa matokeo ya upimaji katika Stadi ya Kuhesabu ulifanyika kwa kila swali kwa kuzingatia vigezo vya utendaji. Pia uchambuzi wa majibu ya wanafunzi ulifanyika kwa kila swali kwa kuzingatia alama walizopata. Aidha, ulinganifu wa umahiri katika utendaji ulifanyika kwa wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza kujifunzia pamoja na wanaosoma katika shule za vijijini na mjini. Kwa ujumla matokeo ya uchambuzi katika stadi hii yanaonesha kuwa wanafunzi 1,059 (17.72%) walikuwa na utendaji hafifu, 1,394 (23.32%) utendaji wa wastani, 2,063 (34.52%) utendaji mzuri na 1,461 (24.44%) utendaji mzuri sana. Sura hii inaeleza muundo wa karatasi ya upimaji, vigezo vya utendaji wa mwanafunzi katika kumudu Stadi ya Kuhesabu na uchambuzi wa majibu ya mwanafunzi.

## 4.2 Muundo wa Karatasi ya Upimaji wa Stadi ya Kuhesabu

Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Pili katika Stadi ya Kuhesabu ulikuwa na maswali ishirini (20) yenye jumla ya alama 50 ambapo kila mwanafunzi alitakiwa kujibu maswali yote.

## 4.3 Vigezo vya Utendaji Katika Stadi ya Kuhesabu

Maeneo yaliyopimwa katika Stadi ya Kuhesabu yalikuwa ni kutambua namba zilizokosekana katika mtiririko wa namba,

kujumlisha, kutoa na kufumbua mafumbo. Kila umahiri katika maeneo hayo ulipimwa kwa maswali matano (5). Upimaji wa viwango vya utendaji kwa kila eneo ulitumia vigezo vinne ambavyo ni utendaji hafifu kwa mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi maswali yasiyozidi mawili (2) katika umahiri husika; utendaji wa wastani kwa mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi maswali matatu (3) katika umahiri husika; utendaji mzuri kwa mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi maswali manne (4) katika umahiri husika na utendaji mzuri sana kwa mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi maswali yote matano (5) katika umahiri husika.

## 4.4 Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi

### 4.4.1 Umahiri wa Kutambua Namba Inayokosekana katika Mtiririko

Upimaji katika eneo hili ulihusisha swali la 1 hadi la 5. Maswali hayo yalipima uwezo wa mwanafunzi wa kusoma na kutambua namba iliyokosekana katika mfuatano wa kuongezeka au kupungua kwa ama hatua 1, 2, 5 au 10 na kisha kuiandika.

Muhtasari wa utendaji katika umahiri huu kwa kutumia vigezo vya utendaji vilivyotajwa umeoneshwa katika safu ya kwanza ya Jedwali Na. 7 linaloonesha utendaji wa jumla wa Stadi ya Kuhesabu.

**Jedwali Na 7: Utendaji wa Jumla wa Stadi ya Kuhesabu**

| Idadi ya Wanafunzi Waliofanya Upimaji wa Stadi ya Kuhesabu (5,977) | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Hafifu 0 - 2 | | Wastani 3 | | Vizuri 4 | | Vizuri sana 5 | |
| **Umahiri** | **Idadi** | **Asilimia** | **Idadi** | **Asilimia** | **Idadi** | **Asilimia** | **Idadi** | **Asilimia** |
| **Namba zinazokosekana** | 2,770 | 46.34 | 1,351 | 22.60 | 851 | 14.24 | 1,003 | 16.78 |
| **Kujumlisha** | 1,500 | 25.10 | 1,231 | 20.60 | 1,594 | 26.67 | 1,652 | 27.64 |
| **Kutoa** | 2,070 | 34.63 | 1,331 | 22.27 | 1,539 | 25.75 | 1,037 | 17.35 |
| **Hesabu za Mafumbo** | 2,273 | 38.03 | 1,088 | 18.20 | 1,149 | 19.22 | 1,467 | 24.54 |


Jedwali Na. 7 linaonesha kuwa jumla ya wanafunzi 5,977 walipimwa katika Stadi ya Kuhesabu. Wanafunzi 2,770 (46.34%) walikuwa na utendaji hafifu, 1,351 (22.60%) utendaji wa wastani, 851 (14.24%) utendaji mzuri na 1,003 (16.78%) walikuwa na utendaji mzuri sana. Takwimu hizi zinaonesha kuwa karibu nusu ya wanafunzi waliofanya swali la 1 hadi 5 walikuwa na utendaji hafifu katika kubaini namba zinazokosekana. Muhtasari wa matokeo ya wanafunzi katika maswali hayo umewasilishwa katika Jedwali Na.8 na Chati Na.12.

**Jedwali Na 8: Wanafunzi Waliojibu Swali la 1 hadi 5 Usahihi**

| Namba ya Swali | Idadi ya Waliofanya Upimaji | Waliojibu kwa usahihi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| **1** | 5,977 | 4,895 | 81.9 |
| **2** | 5,977 | 4,265 | 54.6 |
| **3** | 5,976 | 1,481 | 24.8 |
| **4** | 5,975 | 4,023 | 67.3 |
| **5** | 5,977 | 1,908 | 31.9 |


Jedwali Na. 8 linaonesha kuwa wanafunzi waliojibu swali la 1, 2 na 5 ni 5,977 wakati swali la 3 lilijibiwa na wanafunzi 5,976 na swali la 4 lilijibiwa na wanafunzi 5,975. Chati Na.12 inaonesha vizuri zaidi utendaji huo.

**Chati Na. 12: Umahiri wa Wanafunzi katika Kujibu Swali la 1 hadi 5 kwa usahihi**



Chati Na.12 inaonesha kuwa wanafunzi wengi (81.9%) walijibu kwa usahihi swali namba 1 likifuatiwa na swali namba 4 ambalo asilimia 67.3 ya wanafunzi wote walikuwa na utendaji mzuri. Pia, uchambuzi unaonesha kuwa swali namba 2 lilikuwa na utendaji wa wastani wa asilimia 54.6 ya wanafunzi wote waliojibu swali hilo. Uchambuzi zaidi unaonesha kwamba wanafunzi walikuwa na umahiri wa kiwango cha chini katika swali la 3 na la 5.

Kutokana na matokeo haya, inaonesha kwamba wanafunzi wengi walikuwa na umahiri katika kukamilisha mfuatano wa namba unaoongezeka kwa hatua moja (swali la 1) na ule unaoongezeka kwa hatua kumi (swali la 4). Kielelezo Na. 22 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu vizuri maswali ya kujaza namba iliyokosekana.


1. 6, 7, 8, 9, 10.

2. 15,14, 13, 12, 11.

3. 20, 22, 24, 26, 28.


4. 60, 70, 80, 90,100.

5. 55, 60, 65, 70, 75.

Kielelezo Na. 22: Mwanafunzi aliyebaini namba inayokosekana katika swali la 1 hadi 5 kwa usahihi katika dhana ya namba inayokosekana.

Matokeo haya yanaonesha pia, baadhi ya wanafunzi walishindwa kukamilisha mfuatano wa namba zinazopungua kwa hatua moja (swali la 2) ukilinganisha na umahiri waliouonesha katika swali la 1. Hii inadhihirisha kuwa mpangilio wa namba unaopungua uliwatatiza wanafunzi zaidi kuliko ule wa namba unaoongezeka.

Aidha, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi wengi walikuwa na umahiri mdogo katika kukamilisha mfuatano wa namba zenye achano la mbili (swali la 3) na tano (swali la 5) ukilinganisha na umahiri ulioneshwa katika swali la 4 lenye achano la kumi. Hali hii inaonesha kuwa wanafunzi walikosa umahiri wa kutosha katika mfuatano wa namba zinazopungua au kuongezeka kwa hatua zaidi ya moja. Kielelezo Na. 23 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu baadhi ya maswali.




Kielelezo Na. 23: Mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi swali la 1 na 4 na kushindwa swali la 2, 3 na 5 yaliyohusu dhana ya namba inayokosekana.

### 4.4.2 Umahiri wa Kujumlisha

Umahiri wa mwanafunzi wa kujumlisha namba zenye tarakimu zisizozidi tatu ulipimwa kwa kutumia maswali matano. Umahiri huu ulipimwa katika swali la 6 hadi la 10. Maswali hayo yaligawanywa kama ifuatavyo:

(a) Kujumlisha namba mbili zenye tarakimu moja bila kubeba;

(b) Kujumlisha namba mbili, moja yenye tarakimu mbili na nyingine yenye tarakimu moja bila kubeba;

(c) Kujumlisha namba mbili, moja yenye tarakimu moja na nyingine yenye tarakimu mbili kwa kubeba mara moja;

(d) Kujumlisha namba mbili zenye tarakimu mbili kila moja kwa kubeba mara moja; na

(e) Kujumlisha fedha za Tanzania.


Uchambuzi wa utendaji wa wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi 1,500 (25.10%) walikuwa na utendaji hafifu, 1,231 (20.60%) utendaji wa wastani, 1,594 (26.67%) utendaji mzuri na wanafunzi 1,652 (27.64%) walikuwa na utendaji mzuri sana. Takwimu hizi zinaonesha kwamba wanafunzi 3,246 (54.31%) waliweza kujibu maswali manne hadi matano ya kujumlisha kwa usahihi.

Uchambuzi wa kina kwa kila swali ulifanyika ili kubaini ni maswali yapi yalifanyika kwa usahihi na yale yaliyokuwa na utendaji wa chini zaidi. Matokeo yamewasilishwa kwa muhtasari katika Jedwali Na.9 na Chati Na. 13.

**Jedwali Na 9: Wanafunzi Waliojibu Swali la 6 hadi 10 kwa Usahihi**


| Namba ya Swali | Idadi ya Waliofanya | Waliojibu kwa usahihi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| **6** | 5,977 | 5,483 | 91.7 |
| **7** | 5,977 | 4,697 | 78.5 |
| **8** | 5,977 | 4,194 | 70.2 |
| **9** | 5,977 | 3,283 | 54.9 |
| **10** | 5,977 | 2,528 | 42.3 |

**Chati Na. 13: Wanafunzi Waliojibu Swali la 6 hadi 10 kwa Usahihi**




Jedwali Na. 9 na Chati Na.13 vinadhihirisha kuwa maswali yalipangwa kulingana na ngazi ya ugumu wake. Hii imejionesha katika kupungua kwa viwango vya utendaji kutoka swali moja kwenda jingine. Wanafunzi wengi (91.7%) walionesha umahiri zaidi


katika kujibu swali la 6 ukilinganisha na wanafunzi wachache (42.3%) waliojibu swali la 10 kwa usahihi. Hii imeonesha kuwa kadiri idadi ya tarakimu ilivyoongezeka umahiri ulipungua. Aidha, umahiri wa wanafunzi ulipungua katika hesabu zilizohitaji kubeba kutoka mamoja kwenda makumi. Umahiri ulipungua zaidi kwa wanafunzi katika swali lililohusu kujumlisha fedha ukilinganisha na maswali mengine. Kielelezo Na. 24 na 25 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi kuonesha hali hiyo.



6. 1+ 3 =4.
7. 15+ 4 =19.
8. 26+ 5 =211.
9. 34 + 18 =42.

10. Shilingi 50 + shilingi 100 = shilingi 1050

Kielelezo Na. 24: Mwanafunzi anayesoma katika shule inayotumia lugha ya Kiswahili kufundishia, aliyeshidwa swali la 8 na 9 yaliyohitaji kujumlisha namba kwa kubeba na swali la 10 lilihosu kujumlisha fedha.


Find out the answers:

6. 1+ 3 = 4.

7. 15+ 4 = 9.

8. 26+ 5 = 21.

9. 34 + 18 = 42.

10. 50 shillings + 100 shillings = 600 shillings.

Kielelezo Na. 25 Mwanafunzi anayesoma katika shule inayotumia lugha ya Kiingereza kufundishia aliyeweza kujibu swali moja tu kwa usahihi lililohusu kujumlisha namba mbili zenye tarakimu moja bila kubeba.

### 4.4.3 Umahiri wa Kutoa

Umahiri wa wanafunzi katika kutoa namba zenye tarakimu zisizozidi tatu ulipimwa kwa maswali matano (11 hadi 15). Maswali haya yaligawanyika kama ifuatavyo:

(a) Kutoa namba mbili zenye tarakimu moja;

(b) Kutoa namba mbili, moja yenye tarakimu mbili na nyingine yenye tarakimu moja bila kukopa;

(c) Kutoa namba mbili, moja yenye tarakimu mbili na nyingine yenye tarakimu moja kwa kukopa;

(d) Kutoa namba mbili zenye tarakimu mbili kila moja kwa kukopa mara moja na kutoa fedha za Tanzania.

Uchambuzi wa umahiri wa kutoa unaonesha kuwa wanafunzi 2,070 (34.63%) walikuwa na utendaji hafifu, 1,331 (22.27%) utendaji wa wastani, 1,539 (25.75%)

utendaji mzuri na wanafunzi 1,037 (17.35%) walikuwa na utendaji mzuri sana. Takwimu hizi zinaonesha kuwa karibu theluthi moja ya wanafunzi waliofanya swali la 11 hadi 15 walikuwa na utendaji hafifu.


Ulinganifu uliofanyika wa umahiri wa wanafunzi katika dhana ya kujumlisha na kutoa namba ulibaini kuwa umahiri katika dhana ya kujumlisha uko juu kidogo kuliko dhana ya kutoa. Jumla ya wanafunzi waliokuwa na utendaji wa wastani, mzuri na mzuri sana ni wengi (74.91%) katika dhana ya kujumlisha ukilinganisha na asilimia 65.37 ya wanafunzi waliokuwa na utendaji wa aina hiyo katika dhana ya kutoa.

Uchambuzi ili kubaini ni maswali yapi yalifanyika kwa usahihi zaidi na yale yaliyokuwa na utendaji wa chini zaidi ulifanyika na matokeo yamewasilishwa kwa muhtasari katika Jedwali Na.10 na Chati Na. 14.

**Jedwali Na 10: Wanafunzi Waliojibu Swali la 11 hadi 15 Kwa Usahihi**


| **Namba ya Swali** | **Idadi ya Wanafunzi waliopimwa** | **Waliojibu kwa Usahihi** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| **11** | 5977 | 5045 | 84.6 |
| **12** | 5977 | 4236 | 70.9 |
| **13** | 5977 | 3581 | 59.9 |
| **14** | 5977 | 2711 | 45.4 |
| **15** | 5975 | 1959 | 32.8 |

**Chati Na. 14: Umahiri wa Wanafunzi waliojibu Swali la 11 hadi 15 kwa usahihi**




Jedwali Na. 10 na Chati Na. 14 vinaonesha kuwa umahiri ulipungua kutoka swali la 11 kwenda 15. Wanafunzi wengi (84.6%) waliweza kujibu swali la 11 lililohusisha kutoa namba zenye tarakimu moja, likifuatiwa na swali la 12 ambalo lilihusu kutoa namba yenye tarakimu mbili kwa tarakimu moja bila kukopa. Aidha, kadiri idadi ya tarakimu ilivyoongezeka huku ikihitajika kukopa, umahiri ulipungua zaidi. Hii

inadhihirisha kuwa wanafunzi wanakosa umahiri katika dhana ya kutoa ikiwa tarakimu ni zaidi ya moja na ikiwa kuna dhana ya kutoa kwa kukopa. Pamoja na hayo, dhana ya kutoa fedha imeonekana kuwa na utendaji mdogo ikilinganinishwa na maswali mengine, hali ambayo imejitokeza pia katika dhana ya kujumlisha fedha. Kielelezo Na. 26 na 27 vinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi katika umahiri wa kutoa namba.


11. 7 – 2= 5.
12. 18 – 6 = 12.
13. 24 – 9 = 10
14. 45 – 17 = 27
15. Shilingi 500 – shilingi 250 = shilingi Sh 350

Kielelezo Na. 26: Mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi swali la 11 na 12 lakini alishindwa swali la 13, 14 na 15 kutoka shule inayotumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia.

11. 7 – 2= 5 .

12. 18 – 6 = 12 .

13. 24 – 9 = 14 .

14. 45 - 17 = 27 .

15. 500 shillings - 250 shillings = 350 shillings.

Kielelezo Na. 27: Mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi swali la 11 na 12 lakini alishindwa swali la 13, 14 na 15 kutoka shule inayotumia Kiingereza kufundishia na kujifunzia.

### 4.4.4 Umahiri wa Kufumbua Mafumbo

Maswali ya mafumbo katika upimaji huu yalikuwa ni swali la 16 hadi 20. Maswali haya yalipima umahiri wa kutumia matendo ya kujumlisha na kutoa katika maisha ya kila siku. Ili mwanafunzi aweze kujibu maswali ya mafumbo alipaswa kutambua mahusiano ya vitu halisi na namba.

Matokeo ya uchambuzi wa takwimu yanaonesha kuwa wanafunzi 2,273 sawa na asilimia 38.03 walionesha utendaji hafifu, wanafunzi 1,088 sawa na asilimia 18.20 utendaji wa wastani; wanafunzi 1,149 sawa na asilimia 19.22 utendaji mzuri na wanafunzi 1,467 sawa na asilimia 24.54 walikuwa na utendaji mzuri sana.

Aidha, matokeo ya uchambuzi wa kila swali kuonesha idadi na asilimia ya wanafunzi waliojibu kwa usahihi yameaininshwa katika Jedwali Na. 11 na Chati Na. 15.

**Jedwali Na 11: Wanafunzi Waliojibu kwa Usahihi Maswali ya afumbo**

| Namba ya Swali | Idadi ya wanafunzi Waliopimwa | Waliojibu kwa Usahihi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| **16** | 5,976 | 4,099 | 68.6 |
| **17** | 5,976 | 3,052 | 51.1 |
| **18** | 5,977 | 3,834 | 64.1 |
| **19** | 5,977 | 3,403 | 56.9 |
| **20** | 5,975 | 2,567 | 43.0 |

Jedwali Na. 11 na Chati Na. 15 vinaonesha kuwa swali la 16 lilijibiwa vizuri ukilinganisha na maswali mengine ya mafumbo kwani asilimia 68.6 ya wanafunzi wote walilijibu kwa usahihi. Swali la 18 lilifuatia kwa kujibiwa vizuri ambapo asilimia 64.1 ya wanafunzi wote walilijibu kwa usahihi.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa asilimia 56.9 ya wanafunzi wote walijibu swali la 19 kwa usahihi, likifuatiwa na swali la 17 ambalo ni asilimia 51.1 ya wanafunzi wote waliojibu kwa usahihi. Aidha, swali la 20 lilijibiwa kwa usahihi na wanafunzi wachache (43.0%) ukilinganisha na maswali mengine manne (4) ya mafumbo.


Kutokana na matokeo hayo, inaonekana kwamba wanafunzi wana umahiri zaidi wa kujibu maswali ya

mafumbo yanayohusu dhana ya kujumlisha kuliko dhana ya kutoa. Hii ni kwa sababu swali la 16, 18 na 19 yaliyokuwa yanahusisha mafumbo yanayohitaji mwanafunzi kujumlisha namba, yana utendaji wa juu ukilinganisha na swali la 17 na 20 yaliyohitaji mwanafunzi kutoa namba.


Hata hivyo, ulinganifu wa utendaji wa swali la 16 na 18 unaonesha kuwa idadi ya tarakimu za kujumlisha zilipoongezeka umahiri ulipungua. Aidha, umahiri ulipungua zaidi katika swali la 19 liliohusu kujumlisha fedha.

Ulinganifu wa utendaji katika swali la 17 na 20 unaonesha kuwa, ingawa maswali hayo yalimtaka mwanafunzi kutumia stadi ya kutoa katika mafumbo, umahiri wa wanafunzi ulitofautiana katika maswali hayo. Hali hii inaonesha kwamba, idadi ya tarakimu ilipoongezeka au ilipohusisha suala la kutoa fedha, umahiri wa wanafunzi ulipungua. Chati Na. 15 inaonesha utendaji wa wanafunzi katika swali la 16 na 20.

**Chati Na. 15: Umahiri wa Wanafunzi Waliojibu kwa Usahihi Swali la 16 hadi 20**




Kielelezo Na. 28 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu vizuri swali la 16 hadi 20. Aidha, Kielelezo Na. 29 na 30 kinaonesha sampuli za majibu ya wanafunzi walioshindwa kujibu swali la 17 na 20 kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza kufundishia na kujifunzia.



16. Katika darasa kuna wavulana 7 na wasichana 8. Je, darasa hilo lina jumla ya wanafunzi wangapi?

7
+8
15

17. Mkulima ana maembe 19. Alimgawia rafiki yake maembe 10. Je, mkulima alibakiwa na maembe mangapi?

19
-10
9

18. Kurwa ana nazi 30. Doto ana nazi 40. Jumla wana nazi ngapi?

30
+40
70

19. Mary ana shilingi 150. Rose ana shilingi 200. Je, wana jumla ya kiasi gani cha hela?

150
+200
350

20. Said ana shilingi 350. Alitumia shilingi 250 kununua kalamu. Je, kilibaki kiasi gani cha hela?

350
-250
100

Kielelezo Na. 28: Mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi maswali yote matano.

16. Katika darasa kuna wavulana 7 na wasichana 8. Je, darasa hilo lina jumla ya wanafunzi wangapi?

  7
+8
[15]

17. Mkulima ana maembe 19. Alimgawia rafiki yake maembe 10. Je, mkulima alibakiwa na maembe mangapi?

  19
+10
[29]

18. Kurwa ana nazi 30. Doto ana nazi 40. Jumla wana nazi ngapi?

  30
+40
[70]

19. Mary ana shilingi 150. Rose ana shilingi 200. Je, wana jumla ya kiasi gani cha hela?

  150
+200
  350

20. Said ana shilingi 350. Alitumia shilingi 250 kununua kalamu. Je, kilibaki kiasi gani cha hela?

350
250
600

Kielelezo Na. 29: Mwanafunzi kutoka shule inayotumia Lugha ya Kiswahili kufundishia aliyejibu kwa usahihi mafumbo yaliyohusu dhana ya kujumlisha katika swali la 16,18 na19 lakini alishindwa yaliyohusu dhana ya kutoa katika swali la  17 na 20.

16. In a class there are 7 boys and 8 girls. How many pupils are in that class?

  7
+ 8
 15

17. A farmer has 19 mangoes. She gives her friend 10 mangoes. How many mangoes have remained?

  19
+ 10
  29

18. Kurwa has 30 coconuts. Doto has 40 coconuts. How many coconuts do they have all together?

  30
+ 40
  70

19. Mary has 150 shillings. Rose has 200 shillings. How much money do they have?

  150
+ 200
  350

20. Said has 350 shillings. He used 250 shillings to buy a pen. How much money was left?

  350
+ 250
  600

Kielelezo Na. 30: Mwanafunzi kutoka shule inayotumia Kiingereza kufundishia aliyejibu kwa usahihi mafumbo yaliyohusu dhana ya kujumlisha katika swali la 16,18 na19 lakini alishindwa yaliyohusu dhana ya kutoa katika swali la 17 na 20.

## 4.5 Ulinganifu wa Lugha ya Kufundishia na Mahali Shule ilipo


### 4.5.1 Umahiri kwa Kuzingatia Lugha za Kufundishia

Uchambuzi ulifanyika kulinganisha utendaji wa wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiswahili dhidi ya wale wanaotumia lugha ya Kiingereza. Muhtasari wa taarifa ya ulinganifu umeoneshwa katika Jedwali Na. 12 na 13 na katika Chati Na. 16 na 17.

**Jedwali Na 12: Utendaji wa Wanafunzi katika Stadi ya Kuhesabu kwa Shule Zinazotumia Kiswahili**

| Wanafunzi Wanaotumia Lugha ya Kiswahili (4,670) | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Hafifu 0 - 2 | | Wastani 3 | | Vizuri 4 | | Vizuri sana 5 | |
| Umahiri | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia |
| Namba zinazokosekana | 2,421 | 51.84 | 986 | 21.11 | 581 | 12.44 | 682 | 14.60 |
| Kujumlisha | 1,393 | 29.83 | 1,024 | 21.93 | 1,184 | 25.35 | 1,069 | 22.89 |
| Kutoa | 1,834 | 39.27 | 1,053 | 22.55 | 1,112 | 23.81 | 671 | 14.37 |
| Hesabu za Mafumbo | 1,972 | 42.23 | 753 | 16.12 | 816 | 17.47 | 1,129 | 24.18 |

**Chati Na. 16: Umahiri wa Wanafunzi katika Shule Zinazotumia Kiswahili**





| | Hafifu | Wastani | Vizuri | Vizuri sana |
|---|---|---|---|---|
| Namba inayokosekana | 51.84 | 21.11 | 12.44 | 14.6 |
| Kujumlisha | 29.83 | 21.93 | 25.35 | 22.89 |
| Kutoa | 39.27 | 22.55 | 23.81 | 14.37 |
| Mafumbo | 42.23 | 16.12 | 17.47 | 24.18 |

**Idadi ya Maswali aliyopata mwanafunzi**

**Jedwali Na 13: Utendaji wa Wanafunzi kwa Shule Zinazotumia Kiingereza**

| Wanafunzi Wanaotumia Lugha ya Kingereza (1,307) | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Hafifu 0 - 2 | | Wastani 3 | | Vizuri 4 | | Vizuri sana 5 | |
| Maswali | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia |
| Namba zinazokosekana | 349 | 26.70 | 365 | 27.93 | 270 | 20.66 | 323 | 24.71 |
| Kujumlisha | 107 | 8.19 | 207 | 15.84 | 410 | 31.37 | 583 | 44.61 |
| Kutoa | 236 | 18.06 | 278 | 21.27 | 427 | 32.67 | 366 | 28.00 |
| Hesabu za Mafumbo | 301 | 23.03 | 335 | 25.63 | 333 | 25.48 | 338 | 25.86 |

**Chati Na. 17: Umahiri wa Wanafunzi katika Shule Zinazotumia Kiingereza**



Jedwali Na. 12 na Na. 13 na Chati Na. 16 na Na.17 zinaonesha waliopimwa, kati yao 4,670 walitoka shule zinazofundisha kwa kutumia Kiswahili na 1,307 walitoka shule zinazofundisha kwa kutumia Kiingereza. Ulinganifu wa wastani wa utendaji katika makundi hayo mawili kwa kutumia viwango vya utendaji unaonesha kuwa:

(a) Wanafunzi wenye utendaji hafifu kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiswahili kufundishia ni wengi zaidi (40.79%) ukilinganisha na asilimia 19.00 ya wanafunzi kutoka Shule zinazotumia lugha ya Kiingereza.

(b) Wanafunzi wenye utendaji mzuri ni wengi zaidi (27.55%) kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia ikilinganishwa na asilimia 19.80 ya wanafunzi kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiswahili.

(c) Wanafunzi wenye utendaji mzuri sana kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia ni wengi zaidi (30.80%) ukilinganisha na asilimia 19.01 ya wanafunzi kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiswahili.

Kwa ujumla takwimu hizi zinaonesha kuwa wanafunzi wa shule zinazotumia lugha ya Kiingereza walionesha umahiri mkubwa ukilinganisha na wale wa shule zinazotumia Kiswahili.

### 4.5.2 Umahiri wa Wanafunzi kutokana na shule ilipo

Jumla ya wanafunzi waliofanya upimaji kwa shule za vijijini walikuwa 2,943 wakati wanafunzi wa shule za mjini walikuwa 1,727. Madaraja ya utendaji


yaliyotumika katika ulinganifu wa shule za mjini na vijijini ni 0 – 12 utendaji hafifu, 13 – 25 utendaji wa wastani, 26 – 38 utendaji mzuri na 39 – 50 utendaji mzuri sana. Idadi ya wanafunzi na asilimia ya utendaji wao kwa kila daraja umeoneshwa katika Jedwali Na. 14.

**Jedwali Na 14: Utendaji wa Wanafunzi katika Shule za Mjini na Vijijini**

| **Alama** | **Idadi ya wanafunzi** | | **Umahiri (%)** | |
|---|---|---|---|---|
| | **Mjini** | **Vijijini** | **Mjini** | **Vijijini** |
| 0 - 12 | 255 | 773 | 14.77 | 26.27 |
| 13 - 25 | 449 | 730 | 26.00 | 24.80 |
| 26 - 38 | 619 | 858 | 35.84 | 29.15 |
| 39 - 50 | 404 | 582 | 23.39 | 19.78 |
| **Jumla** | **1727** | **2943** | **100.00** | **100.00** |

Aidha, Chati Na. 18 imeonesha kwa ufasaha zaidi utendaji wa wanafunzi walioonеshwa katika Jedwali Na. 14.

**Chati Na. 18: Ulinganifu wa Umahiri kwa Shule za Mjini na Vijijini Zinazofundisha kwa Lugha ya Kiswahili**




Jedwali Na.14 na Chati Na. 18 vinaonesha kuwa wanafunzi wengi wa shule za vijijini wameonesha kuwa na utendaji hafifu zaidi ikilinganishwa na wanafunzi wachache wa shule za mjini. Pia, wanafunzi wengi wa shule za mjini wameonesha kuwa na utendaji wa juu katika viwango vya wastani, vizuri na vizuri sana.

### 4.5.3 Utendaji kwa Shule za Mjini na Shule za Vijijini


Idadi ya wanafunzi waliofanyiwa upimaji kwa shule za vijijini ilikuwa 615 wakati wanafunzi wa shule za mjini ilikuwa 692. Idadi ya wanafunzi na asilimia kuonesha utendaji wao kwa kila daraja umeoneshwa katika Jedwali Na. 15.

**Jedwali Na 15: Utendaji katika Stadi ya Kuhesabu kwa Shule za Mjini na Vijijini**

| Alama | Idadi ya wanafunzi | | Umahiri (%) | |
|---|---|---|---|---|
| | **Mjini** | **Vijijini** | **Mjini** | **Vijijini** |
| 0 - 12 | 18 | 18 | 2.60 | 2.93 |
| 13 - 25 | 130 | 83 | 18.79 | 13.50 |
| 26 - 38 | 312 | 271 | 45.09 | 44.07 |
| 39 - 50 | 232 | 243 | 33.53 | 39.51 |
| **Jumla** | **692** | **615** | **100.00** | **100.00** |

Aidha, Chati Na. 19 imeonesha kwa ufasaha zaidi umahiri wa wanafunzi waliooneshwa katika Jedwali Na. 15.

**Chati Na. 19: Umahiri wa Wanafunzi Utendaji kwa Shule za Mjini na Vijijini Zinazotumia Lugha ya Kiingereza**




Jedwali Na.15 na Chati Na. 19 vinaonesha kuwa, umahiri wa wanafunzi wa vijijini na mjini unapishana kwa kiwango kidogo. Hata hivyo, wanafunzi waliokuwa na Utendaji hafifu wameonesha kuwa na tofauti ndogo sana (0.33%) hali inayoonesha kuwa umahiri wa utendaji wa wanafunzi hautegemei lugha pekee isipokuwa mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

### 4.5.4 Muhtasari wa Uchambuzi katika Stadi ya Kuhesabu

Kwa ujumla matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa wanafunzi wengi walikuwa na umahiri mkubwa katika kukamilisha mfuatano wa namba unaoongezeka kwa hatua moja na ule unaoongezeka kwa hatua kumi, kujumlisha na kutoa namba mbili zenye tarakimu moja bila kubeba na kufumbua mafumbo yaliyohusisha dhana na kujumlisha namba.

Kwa upande mwingine matokeo ya uchambuzi wa takwimu yanaonesha kuwa wanafunzi wengi walikuwa na umahiri mdogo katika kukamilisha mfuatano wa namba zenye kuruka kwa hatua mbili na kuruka kwa hatua tano, kujumlisha na kutoa namba mbili zenye tarakimu mbili kila moja, kujumlisha na kutoa fedha na kufumbua mafumbo yaliyohusisha dhana ya kutoa namba.

# SURA YA TANO

# UCHAMBUZI WA TAARIFA ZA USIMAMIZI

## 5.1 Utangulizi

Dodoso kwa ajili ya Walimu Wakuu na Wasimamizi wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu liliandaliwa. Dodoso hizo ziliwataka Walimu Wakuu na Wasimamizi wa Stadi za KKK kutoa maelezo mbalimbali kuhusu mahudhurio ya wanafunzi, mazingira ya shule na ujuzi wa walimu katika Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Lengo la dodoso hilo lilikuwa kupata taarifa kuhusu ujuzi wa walimu katika kufundisha stadi za KKK na uwepo wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na hali ya mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa ujumla.

## 5.2 Ujuzi wa kufundisha na Mafunzo ya Walimu katika Stadi za KKK

Takwimu zinaonesha kuwa kati ya wasimamizi 771 walioteuliwa, wasimamizi 555 (71.9%) walijaza dodoso na kurudisha. Kati yao wasimamizi 529 sawa na asilimia 95.3 walieleza kuwa wanafundisha Darasa la 1 au la 2 na kwamba asilimia 77.1 ya walimu hao walithibitisha kupewa mafunzo ya kufundisha stadi za KKK. Hivyo, kuwepo kwa asilimia 77.98 ya wanafunzi wenye umahiri katika stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu kuna mahusiano na suala la walimu kufundisha vizuri kwa kuwa walimu walio wengi walihudhuria mafunzo ya stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.


Jedwali Na. 16 linaonesha maoni ya wasimamizi kuhusu ufundishaji, mafunzo ya walimu na muda uliotumika kupima stadi za KKK.

**Jedwali Na 16: Ufundishaji, Mafunzo na Muda Uliopangwa wa Upimaji wa KKK**

| Na | Swali | Idadi | Ndiyo | % | Hapana | % | Wasiojibu | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Je unafundisha KKK katika darasa la 1 au 2? | 555 | 529 | 95.3 | 18 | 3.2 | 8 | 1.4 |
| 2. | Je umewahi kupata mafunzo ya KKK? | 555 | 398 | 71.7 | 149 | 26.8 | 08 | 1.4 |
| 3. | Muda uliopangwa wa upimaji kwa KKK unatosheleza? | 555 | 441 | 79.5 | 85 | 15.3 | 29 | 5.2l |

## 5.3 Mahudhurio ya Wanafunzi

Uchambuzi wa taarifa za wasimamizi umeonesha kuwa asilimia 86 ya wanafunzi ambao hawakushiriki upimaji walikuwa watoro. Wanafunzi wengine (8%) walikuwa wagonjwa na asilimia 6 hawakuhudhuria kwa sababu nyinginezo zikiwemo kuhama kwa wazazi wao pamoja na kifo. Chati Na. 20 inaonesha asilimia ya wanafunzi ambao hawakushiriki katika upimaji na sababu za kutoshiriki kwao.




Chati Na. 20: inaonesha utoro kuwa ndiyo sababu kubwa iliyofanya wanafunzi wasishiriki katika upimaji wa majaribio wa Darasa la Pili.

## 5.4 Vifaa, Mazingira ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Takwimu zinaonesha kuwa, asilimia 57.4 ya wasimamizi waliripoti kuwa shuleni kwao hakuna vitabu vya kufundishia stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Aidha, kwa wale walioripoti kuwepo kwa vitabu shuleni kwao (85%) walieleza kuwa havitoshelezi. Aidha, kuhusu kuwepo kwa muhtasari wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu asilimia 84.1 walijibu kuwa ipo na asilimia 15.9 walieleza kuwa hawakuwa na muhtasari.

Walimu Wakuu walipoulizwa kuhusu kuwepo kwa madawati ya kutosheleza katika shule zao, asilimia 43.2 walijibu ndiyo na asilimia 56.8 walijibu hapana. Kwa kuzingatia majibu yaliyotolewa na Walimu Wakuu kuhusu vifaa na mazingira ya kufundishia na kujifunzia, ni wazi kuwa ukosefu wa vitabu unaweza kuwa sababu ya utendaji uliojitokeza. Aidha, asilimia ndogo (15.9%) walionesha kutokuwa na mihtasari ambacho ni kiashiria kuwa walimu hao wanafundisha bila

miongozo na hivyo kusababisha wanafunzi kutopata umahiri uliokusudiwa.

Majibu ya Walimu Wakuu yanaonesha idadi ya madawati haitoshelezi katika shule nyingi. Aidha, walimu wakuu wengi waliripoti kutokuwa na vitabu vya kufundishia na walionavyo havitoshelezi. Mambo haya mawili yanaweza kuwa yamechangia katika kufanya mazingira ya kufundishia na kujifunzia kuwa na changamoto na hivyo kutofikiwa viwango vya juu vya umahiri wa utendaji katika stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Jedwali Na. 17 linaonesha maoni ya walimu wakuu kuhusu vifaa, mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

**Jedwali Na 17: Maoni ya Walimu Wakuu**

| Na. | Swali | Ndiyo | (%) | Hapana | (%) | Hawakujibu |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Je shule ina Muhtasari wa KKK? | 37 | 84.1 | 07 | 15.9 | 03 |
| 2. | Je unavyo vitabu vya kufundishia KKK katika shule yako? | 20 | 42.6 | 27 | 57.4 | 00 |
| 3. | Je vitabu hivyo vinatosheleza kwa kila mwanafunzi? | 03 | 15 | 17 | 85 | 00 |
| 4. | Idadi ya madawati yaliyopo yanatosheleza kwa kila mwanafunzi? | 19 | 43.2 | 25 | 56.8 | 00 |

# SURA YA SITA

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 6.1 Hitimisho

Kwa ujumla, wanafunzi walionesha kuwa na utendaji mzuri katika stadi zote tatu. Hata hivyo, katika Stadi ya Kusoma asilimia 10.13 ya wanafunzi walishindwa kusoma maneno yenye herufi mwambatano na kushindwa kujibu maswali ya ufahamu. Katika Stadi ya Kuandika asilimia 11.68 ya wanafunzi walishindwa kuandika, kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za usomaji kwa usahihi kwa sababu ya kutokuwa na umahiri wa kuumba herufi za silabi mwambatano. Katika Stadi ya Kuhesabu baadhi ya wanafunzi (17.72%) hawakufanya vizuri kwa sababu hawakuwa na maarifa katika hesabu za kubaini namba inayokosekana katika mfululizo wa namba zinazoongezeka au kupungua kwa hatua zaidi ya moja na kukosa umahiri katika hesabu za matendo ya kujumlisha na kutoa katika hatua ya pili.

Aidha shule zinazofundisha kwa kutumia lugha ya Kiingereza zilifanya vizuri zaidi ukilinganisha na shule zinazotumia lugha ya Kiswahili. Aidha, shule za mjini zilikuwa na utendaji mzuri zaidi ukilinganisha na shule za vijijini.

Matokeo ya uchambuzi wa taarifa za wasimamizi yanaonesha kuwa baadhi ya shule zilizofanyiwa upimaji zilionesha kuwepo changamoto mbalimbali kama vile upungufu wa vitabu vya kufundishia, mihtasari, madawati na baadhi ya walimu kutokupata mafunzo ya kufundisha stadi za KKK. Baraza la Mitihani linaamini kuwa Wadau mbalimbali wa elimu wakiwemo walimu wakuu na walimu wanaohusika katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za Kusoma, Kuandika, Kuhesabu wakifanyia kazi changamoto zilizobainishwa katika taarifa hii umahiri wa utendaji wa wanafunzi katika Darasa la Pili utaimarika. Kwa kufanya hivyo viwango vya utendaji wa wanafunzi katika ngazi zingine za elimu utaimarika zaidi.

## 6.2 Mapendekezo

Ili kuongeza umahiri wa wanafunzi katika kumudu stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Baraza la Mitihani linapendekeza yafuatayo:

(a) Wizara ya Elimu Sayansi, Teknolojia na Ufundi ifanye ufuatiliaji kuboresha ufundishaji na ujifunzaji katika stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu na hivyo kuinua zaidi kiwango cha umahiri cha wanafunzi katika stadi hizo.

(b) Katika kuwajengea wanafunzi uwezo wa kumudu stadi za KKK, walimu wakuu waweke mikakati madhubuti ya kuhakikisha kuwa wanafunzi wa Darasa la Kwanza na la Pili wanafundishwa kwa ufasaha stadi zote kwa kuzingatia matakwa ya mtaala na muhtasari wa stadi za KKK. Aidha, wafanye ufuatiliaji kuhusu suala zima la mahudhurio ya wanafunzi shuleni ili wanafunzi wote wanaokuwa wameandikishwa Darasa la Kwanza waweze kusoma na kupata stadi na maarifa yanayotakiwa katika mtaala.

(c) Walimu wanaofundisha stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu waweke mkazo zaidi katika maeneo yafuatayo: stadi za Kusoma (Ufahamu), Kuandika (uumbaji wa herufi mwambatano na matumizi ya alama za uandishi) na Kuhesabu (namba zinazokosekana na hesabu za kujumlisha na kutoa katika hatua ya pili). Aidha, walimu wanashauriwa kuwa wabunifu katika kuandaa zana za kufundishia na kujifunzia ili kuwasaidia wanafunzi kumudu zaidi stadi za KKK na hivyo kuwajengea umahiri wa viwango vya juu vya utendaji.

(d) Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na ufundi pamoja na ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na wadau wengine wa elimu, ihakikishe kuwa vitendea kazi vya kutosha kama vile vitabu,

mihtasari na madawati vinakuwepo shuleni. Aidha, walimu wakuu wahakikishe vitendea kazi hivyo vinatunzwa na kutumika ipasavyo.

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## BARAZA LA MITIHANI
## UPIMAJI WA ELIMU YA MSINGI DARASA LA PILI

201 STADI YA KUSOMA

Muda: Dakika 15 Jumanne, 24 Novemba 2015 asubuhi

### Maelekezo

1. Karatasi hii ina **maswali matatu**.

2. Mwanafunzi anatakiwa kujibu maswali **yote** kwa kusoma.

3. Kila mwanafunzi atapimwa kwa **dakika 15**.

4. Msimamizi anatakiwa kujaza taarifa za mwanafunzi katika nafasi zilizo wazi kwenye kona ya juu ya kulia mwa karatasi ya skeli ya upimaji kwa **kalamu ya wino wa bluu**.

5. Mwanafunzi atakapokuwa amemaliza kusoma, msimamizi anatakiwa kujaza alama katika **karatasi maalum** ya skeli ya upimaji aliyopewa kwa kutumia **kalamu ya wino mwekundu**.

## Kusoma Maneno

Mwongoze mwanafunzi kusoma maneno kwa kuzingatia yafuatayo:

(a) Mwoneshe mwanafunzi (kwa kugusa kwa kalamu) kuanzia neno la kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari.

(b) Mwelekeze mwanafunzi kusoma maneno kwa sauti, umakini na haraka kadri awezavyo.

(c) Hakikisha kuwa mwanafunzi anatumia **sekunde tatu** tu kusoma neno. Baada ya sekunde tatu mwelekeze mwanafunzi kusoma neno linalofuata.

(d) Usomaji wa maneno yote utafanyika kwa **dakika tatu**, ambapo **dakika moja** itatumiwa na mwanafunzi katika usomaji na **dakika mbili** zitatumiwa na msimamizi katika ukokotoaji wa alama na ujazaji wa karatasi ya skeli ya upimaji.

1. Mwanafunzi asome maneno yafuatayo:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Jua | asubuhi | tano | simba | mchezo |
| wazazi | chungwa | shati | watu | weka |
| kimbia | panya | vitabu | siku | kijani |
| tisa | rubani | maji | asante | mguu |

## Kusoma Sentensi

Mwongoze mwanafunzi kusoma sentensi kwa kuzingatia yafuatayo:

(a) Mwoneshe mwanafunzi (kwa kugusa kwa kalamu) kuanzia sentensi ya kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari.

(b) Mwelekeze mwanafunzi kusoma sentensi kwa sauti, umakini na haraka kadri awezavyo.

(c) Hakikisha kuwa mwanafunzi anatumia **sekunde tatu** tu kusoma neno. Baada ya sekunde tatu mwelekeze mwanafunzi kusoma neno linalofuata.

(d) Usomaji wa sentensi zote utafanyika kwa **dakika nne**, ambapo **dakika moja** itatumiwa na mwanafunzi katika usomaji na **dakika tatu** zitatumiwa na msimamizi katika ukokotoaji wa alama na ujazaji wa karatasi ya skeli ya upimaji.

2. Mwanafunzi asome sentensi zifuatazo:

| |
|---|
| Magari ni mazuri sana. |
| Wazazi wangu ni wakarimu. |
| Mwalimu wetu ni mzuri. |
| Mimi nilifua nguo zangu. |
| Tanzania ni nchi yangu. |

## Kusoma Kifungu cha Maneno

Mwongoze mwanafunzi kusoma kifungu cha maneno kwa kuzingatia yafuatayo:

(a) Mwoneshe mwanafunzi kifungu cha maneno (kwa kugusa kwa kalamu) kuanzia sentensi ya kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari na

mweleze mwanafunzi kuwa akimaliza kusoma, utachukua karatasi na utamuuliza maswali yanayohusiana na habari aliyoisoma.

(b) Mwelekeze mwanafunzi kusoma kifungu cha maneno kwa sauti, umakini na haraka kadri awezavyo. Mwanafunzi atakapokuwa anasoma, fuatilia usomaji wake kwa kutumia kifungu cha maneno kilichopo katika Skeli ya Upimaji.

(c) Mwanafunzi akimaliza kusoma chukua karatasi yake kisha muulize maswali yaliyopo katika **karatasi maalum** ya skeli ya upimaji uliyopewa.

(d) Usomaji wa kifungu cha maneno utafanyika kwa **dakika nane**, ambapo dakika **tatu** zitatumiwa na mwanafunzi katika usomaji na dakika **tano** zitatumiwa na msimamizi katika kuuliza maswali kwa mdomo, ukokotoaji wa alama na ujazaji wa karatasi ya skeli ya upimaji.

3. Mwanafunzi asome kifungu cha maneno kifuatacho kisha ajibu maswali atakayoulizwa kwa mdomo:

Baraka na Tumaini ni marafiki, wanaishi kijiji cha Mtakuja.
Watoto hawa wanasoma katika shule ya msingi Mtakuja.
Wote wako darasa la pili. Walimu wao wanawapenda sana,
kwa sababu wana akili. Katika matokeo ya muhula uliopita,
Tumaini alikuwa wa kwanza. Rafiki yake alikuwa wa pili
darasani kwao. Wote wawili walifurahi sana. Katika sherehe
ya kufunga shule, wote wawili waliopewa zawadi nzuri.

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

## THE NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

## STANDARD TWO PRIMARY EDUCATION ASSESSMENT

## 201 READING SKILLS

Time: 15 Minutes Tuesday, 24th November 2015 a.m

### Instructions

1. *This paper has* **three** *questions.*
2. *The pupil is required to answer* **all** *questions by reading.*
3. *Every Pupil will be assessed for* **15 minutes**.
4. *The invigilator is required to fill the pupil's information on the blank spaces at the top most corner on the right hand side of the Assessment Scale by using* **blue pen**.
5. *When the pupil has finished the reading, the invigilator is required to fill in the marks on the special assessment scale paper given by using a* **red pen**.

### Reading of words

*Guide the pupil to read words by considering the following:*

*(a) Show the pupil (by pointing with a pen) starting from the first word from left to right in each row.*

(b) Instruct the pupil to read words loudly, carefully and as quickly as possible.

(c) Make sure that the pupil use only **three seconds** in reading each word. After three seconds, instruct the pupil to read the next word.

(d) Reading of all words will take **three minutes**, in which **one minute** will be used by the pupil to read and **two minutes** will be used by the invigilator to calculate marks and fill in the assessment scale paper.

1. The pupil should read the following words:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| sun | morning | five | lion | game |
| parents | orange | shirt | people | put |
| run | rat | books | day | green |
| nine | pilot | water | thanks | foot |

## Reading of Sentences

Guide the pupil to read sentence by considering the following:

(a) Show the pupil (by pointing with a pen) starting from the first sentence from left to right in each row.

(b) Instruct the pupil to read five sentences loudly, carefully and as quickly as possible.

(c) Make sure that the pupil use only **three seconds** in reading each word in a sentence. After three seconds, instruct the pupil to read the next word.

(d) Reading of all sentences will be done for **four minutes**, in which **one minute** will be used by the pupil to read and **three minutes** will be used by the invigilator to calculate marks and fill in the assessment scale paper.

2. The pupil should read the following sentences:

| |
|---|
| Cars are very nice. |
| My parents are kind. |
| Our teacher is good. |
| I washed my clothes. |
| Tanzania is my country. |

## Reading of a Paragraph

Guide the pupil to read paragraph by considering the following:

(a) Show the pupil the paragraph (by pointing with a pen) starting from the first sentence from left to right in each row and also tell the pupil that when he/she has finished the reading, you will take his/her paper and ask him/her questions which are related to the paragraph.

(b) Instruct the pupil to read the paragraph loudly, carefully and as quickly as possible. When the pupil is reading, trace his/her reading by using the paragraph which is in the assessment scale.

(c) When the pupil has finished reading, take his/her assessment paper which he/she was reading and ask him/her questions given in a special assessment scale.

(d) Reading of the paragraph will take **eight minutes**, in which **three minutes** will be used by the pupil to read and **five minutes** will be used by the invigilator to ask oral question, calculate marks and to fill in the assessment scale paper.

3. The pupil should read the following paragraph and answer orally the questions which the teacher will ask:

Baraka and Tumaini are friends. They are in standard two at Mtakuja primary school. Their teachers' like them because they are clever. In the last term test results, Tumaini was the first. His friend was the second in their class. They were happy. At the end of the year, there was a party. In that party they were given nice gifts.

# BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

## Fomu ya Kujaza Alama za Mwanafunzi kwa Upimaji wa Kusoma

Jina la Mwanafunzi____________________

Namba ya Mwanafunzi________________

Jina la Shule___________________________

Wilaya_______________________________

Mkoa________________________________

| KWA MATUMIZI YA MPIMAJI TU | | |
|---|---|---|
| Namba ya Swali | Alama | Saini ya Mpimaji |
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| Jumla | | |

1. Kusoma maneno (alama 10).

Weka alama ya **mkwaju (/)** kwa maneno yote ambayo mwanafunzi **ameshindwa** kuyasoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi aliposahihisha kusoma neno alilokuwa amekosea, zungushia **(Ø)** neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi **alama 00$^1/_2$**).

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| jua | asubuhi | tano | simba | mchezo |
| wazazi | chungwa | shati | watu | weka |
| kimbia | panya | vitabu | siku | kijani |
| tisa | rubani | maji | asante | mguu |

**Alama:**

2. Kusoma sentensi (alama 20).

Weka alama ya **mkwaju (/)** kwa maneno yote katika sentensi ambayo mwanafunzi **ameshindwa** kuyasoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi aliposahihisha kusoma neno alilokuwa amekosea, zungushia **(Ø)** neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi **alama 01**).

Magari ni mazuri sana.

Wazazi wangu ni wakarimu.

Mwalimu wetu ni mzuri.

Mimi nilifua nguo zangu.

Tanzania ni nchi yangu

**Alama:**

3. Kusoma kifungu cha maneno kisha kujibu maswali kwa mdomo (alama 20).

   Sikiliza kwa makini usomaji wa mwanafunzi, baada ya mwanafunzi kusoma, chukua karatasi aliyokuwa anasoma kisha muulize maswali yaliyoko chini ya kifungu cha maneno.

   Baraka na Tumaini ni marafiki, wanaishi kijiji cha Mtakuja.Watoto hawa wanasoma katika shule ya msingi Mtakuja. Wote wako darasa la pili. Walimu wao wanawapenda sana, kwa sababu wana akili. Katika matokeo ya muhula uliopita,Tumaini alikuwa wa kwanza. Rafiki yake alikuwa wa pili darasani kwao. Wote wawili walifurahi sana. Katika sherehe ya kufunga shule, wote wawili waliopewa zawadi nzuri.

## Maswali na Majibu

Endapo mwanafunzi atatoa jibu sahihi, zungushia alama **5** na iwapo mwanafunzi atatoa jibu lisilo sahihi zungushia alama **0** na kisha andika jumla ya alama kwenye jedwali lifuatalo:

| Na. | Maswali na Majibu | alama | |
|---|---|---|---|
| (a) | Rafiki yake Tumaini anaitwa nani? **(Baraka)** | 5 | 0 |
| (b) | Baraka na Tumaini wanasoma darasa gani? **(Darasa la Pili)** | 5 | 0 |
| (c) | Nani alikuwa wa kwanza katika matokeo ya muhula uliopita? **(Tumaini)** | 5 | 0 |
| (d) | Kwa nini walimu wanawapenda Baraka na Tumaini? **(kwa sababu wana akili)** | 5 | 0 |
| | **Jumla** | | |

**Maoni ya msimamizi kuhusu usomaji wa mwanafunzi:**

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

__________________________________________

**Jina na Sahihi ya Msimamizi:**_____________________________

**Shule Anayotoka:**___________________________________

**Anuani:**_______________________________________

Namba ya Simu:_______________________________________________

Tarehe:___________________________________________________________

**Kiambatanisho Na. 4: Assessment Scale**

# THE NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL OF TANZANIA

## The Form to Fill in Pupil's Marks for Reading Assessment

Name of the Pupil_______________________________

Pupil's Number _______________________________

Name of the School_____________________________

District _______________________________________

Region_________________________________________

| FOR ASSESSOR'S USE ONLY | | |
|---|---|---|
| Question number | Marks | Assessor's Signature |
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| Total | | |

1. Reading of words (10 marks)

Put a **stroke mark (/)** in all words which the pupil has failed to read and circle **(Ø)** self-correction if you already marked the word incorrect. (Each correct word is a **00$^1/_2$ mark)**.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| sun | morning | five | lion | game |
| parents | orange | shirt | people | put |
| run | rat | books | day | green |
| nine | pilot | water | thanks | foot |

**Marks:**

2. Reading of the sentences (20 marks)

Put a **stroke mark (/)** in all words in a sentence which the pupil has failed to read and circle **(Ø)** self-correction if you already marked the word in a sentence incorrect. (Each correct word in a sentence is a **01 mark**).

| |
|---|
| Cars are very nice. |
| My parents are kind. |
| Our teacher is good. |
| I washed my clothes. |
| Tanzania is my country. |

**Marks:**

3. *Reading of the paragraph and answering the questions orally (20 marks).*
*Listern carefully while the pupil is reading the paragraph. When he/she has finished reading, take the paper which the pupil was reading and then ask him/her questions which are below the paragraph.*

Baraka and Tumaini are friends. They are in standard two at Mtakuja primary school. Their teachers' like them because they are clever. In the last term test results, Tumaini was the first. His friend was the second in their class. They were happy. At the end of the year, there was a party. In that party they were given nice gifts.

## Questions and Answers

*If the pupil will give a correct answer, circle 5 marks and if he/she will give incorrect answer, circle 0 mark and then write a total marks in the space provided in the table.*

| No. | Questions and Answers | Marks | |
|---|---|---|---|
| (a) | *Who is Tumaini's friend?* **(Baraka)** | 5 | 0 |
| (b) | *In what class is Baraka and Tumaini?* **(Standard two)** | 5 | 0 |
| (c) | *Who was the first one in the last term results?* **(Tumaini)** | 5 | 0 |
| (d) | *Why do teachers like Baraka and Tumaini?.* **(Because they were clever)** | 5 | 0 |
| | **Total** | | |

Invigilators comments on the reading of a pupil's

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

___

Name and Signature of the Invigilator:__________________________

Working Station:______________________________________

_____

Address:_____________________________________

____________

Telephone Number:_____________________________________

___

Date:_______________________________________________

_____

Jina la Mwanafunzi _____________

Namba ya Mwanafunzi___________

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BARAZA LA MITIHANI
UPIMAJI WA ELIMU YA MSINGI DARASA LA PILI

202 STADI ZA KUANDIKA

Muda: Dakika 40 Jumatatu, 23 Novemba 2015 asubuhi

## Maelekezo

6. Karatasi hii ina **maswali matatu**.
7. Andika **Jina lako** na **Namba yako** katika ukurasa wa kwanza.
8. Jibu maswali **yote** matatu.
9. Andika **majibu yako yote** kwa kutumia penseli.

| KWA MATUMIZI YA MPIMAJI TU | | |
|---|---|---|
| Namba ya Swali | Alama | Saini ya Mpimaji |
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| Jumla | | |

1. **Sikiliza** kwa makini maneno yanayosomwa na mwalimu kisha **andika maneno hayo kwa usahihi** katika nafasi zilizo wazi:

(a) ______________________________

(b) ______________________________

(c) ______________________________

(d) ______________________________

(e) ______________________________

(f) ______________________________

(g) ______________________________

(h) ______________________________

(i) ______________________________

(j) ______________________________

2. **Andika** maneno yafuatayo kwa **herufi kubwa** katika nafasi iliyo wazi.

(a) ua______________________________

(b) nyeusi______________________________

(c) mmea______________________________

(d) kijiko______________________________

(e) gari______________________________

(f) mlango______________________________

(g) chupa______________________________

(h) nyumba______________________________

(i) dhahabu______________________________

(j) shindwa______________________________

3. **Nakili** kifungu cha maneno kifuatacho na weka alama za **nukta (.): mkato (,): alama ya kushangaa (!)** na **alama ya kuuliza (?)** kwa usahihi.

Furaha alinunua nini sokoni jana_______ Alinunua maembe______machungwa na ndizi______ Oh_____ yalikuwa matunda matamu sana______

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BARAZA LA MITIHANI

# UPIMAJI WA ELIMU YA MSINGI DARASA LA PILI

## 202 MANENO YA IMLA

### Maelekezo kwa Msimamizi

1. Tumia **dakika kumi** kusoma imla kwa wanafunzi katika swali la 1.
2. Soma maneno ya Imla kwa **sauti** na kwa **umakini**.
3. Waelekeze wanafunzi kuwa utasoma kila neno **mara mbili** hivyo wasikilize kwa makini
4. Waelekeze wanafunzi kuwa maneno yote yatatakiwa kuandikwa kwa **herufi ndogo**.
5. Soma taratibu neno moja **mara mbili** na kuweka **pumziko** la **sekunde 20** ili wanafunzi waweze kuandika neno ulilosoma.
6. Soma tena maneno **yote** kwa **mara ya mwisho** ili wanafunzi wafanye marekebisho ya maneno waliyokosea kuandika.

# IMLA

| | | |
|---|---|---|
| (a) ndege | (b) shoka | (c) inzi |
| (d) saa | (e) taa | (f) viatu |
| (g) chumba | (h) gauni | (i) nyeusi |
| (j) meza | | |

Pupil's Name________________________

Pupils Number_______________________

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

## NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL OF TANZANIA
## STANDARD TWO PRIMARY EDUCATION ASSESSMENT

## 202 WRITING SKILLS

Time: 40 Minutes Wednesday, 23rd October 2015 a.m.

### Instructions

1. *This paper has* **three questions**.
2. *Write your* **Name** *and* **Number** *on the first page.*
3. *Answer* **all** *three questions.*
4. *Write* **all** *your* **answers** *in* **pencil**.

| FOR ASSESSOR'S USE ONLY | | |
|---|---|---|
| Question Number | Marks | Assessor's Signature |
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| TOTAL | | |
| | | |

1. **Listen carefully** *to the words being read by the*

teacher and then **write** those words correctly in the spaces provided:

(a) ______________________________

(b) ______________________________

(c) ______________________________

(d) ______________________________

(e) ______________________________

(f) ______________________________

(g) ______________________________

(h) ______________________________

(i) ______________________________

(j) ______________________________

2. **Write** the following words in **capital letters** in the spaces provided.

(a) flower ______________________________

(b) black______________________________

(c) plant______________________________

(d) spoon______________________________

(e) car______________________________

(f) door________________________________

(g) bottle________________________________

(h) house________________________________

(i) gold________________________________

(j) fail________________________________

3. **Copy** the following paragraph and then put **full stop (.)**: **comma (,)**: **exclamation mark (!)** and **question mark (?)** correctly.

What did Furaha buy yesterday_______ She bought mangoes _____ oranges and bananas______ Oh_______ they were sweet______

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

________________________________

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

## NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL OF TANZANIA
## STANDARD TWO PRIMARY EDUCATION ASSESSMENT

---

202 WRITING SKILLS

## WORDS FOR DICTATION

### Instructions to the Invigilator

1. Use **ten minutes** to read the **dictation** for question 1 to the normal sighted pupils and **fifteen minutes** to the visual impaired pupils.
2. Read the words for dictation **loudly** and **carefully**.
3. Tell the pupils that you will read each word **two times**and that each pupil should **listen carefully.**
4. Tell the pupils that they should write the words read in **small letters**.
5. Read one word **two times** slowly and **pause** for **20 seconds**for thenormal sighted pupilsand **twenty five minutes** for the visual impaired pupilsto **write** the word read.
6. Read the words **forthe last time** so that the pupils can make corrections where necessary.

# DICTATION

(a) bird

(b) axe

(c) fly

(d) watch

(e) lamp

(f) shoes

(g) room

(h) dress

(i) black

(j) table

**Kiambatisho Na 9: Stadi ya Kuhesabu**

Jina la

Mwanafunzi..................................

......

Namba ya

Mwanafunzi..................................

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

UPIMAJI WA TAIFA DARASA LA PILI

203 STADI YA KUHESABU

Muda: Saa 1 Jumatatu, 23 Novemba 2015 Asubuhi

---

## Maelekezo

1. Karatasi hii ina maswali **20**.
2. Jibu maswali **yote**.
3. Andika majibu **yote** kwa **penseli**.
4. Andika **namba** yako na **jina** lako katika ukurasa wa kwanza.

| KWA MATUMIZI YA MPIMAJI TU | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Namba ya Swali | Alama | Saini ya Mpimaji | Namba ya Swali | Alama | Saini ya Mpimaji | Namba ya Swali | Alama | Saini ya Mpimaji | Namba ya Swali | Alama | Saini ya Mpimaji |
| 1. | | | 7. | | | 13. | | | 19. | | |
| 2. | | | 8. | | | 14. | | | 20. | | |
| 3. | | | 9. | | | 15. | | | | | |
| 4. | | | 10. | | | 16. | | | | | |
| 5. | | | 11. | | | 17. | | | | | |

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 6. | | | 12. | | | 18. | | | | | |

*Kamilisha mfuatano wa namba zifuatazo kwa kuandika namba inayokosekana.*

1. 6, 7, 8, _____, 10.
2. 15,14, 13, 12, _____.
3. 20, 22, 24, _____,28.
4. 60, _____, 80, 90,100.
5. 55, 60, _____, 70, 75.

*Tafuta majibu:*

6. 1+ 3 = ______.
7. 15+ 4 = ______.
8. 26+ 5 = _______.
9. 34 + 18 = _______.
10. *Shilingi* 50 + *shilingi* 100 = *shilingi* _______.
11. 7 – 2= _______.
12. 18 – 6 = _______.
13. 24 – 9 = _______.
14. 45 – 17 = _________.
15. *shilingi* 500 – *shilingi* 250 = *shilingi* __________.
16. Katika darasa kuna wavulana 7 na wasichana 8. Je, darasa hilo lina jumla ya wanafunzi wangapi?
17. Mkulima ana maembe 19. Alimgawia rafiki yake maembe 10. Je, mkulima alibakiwa na maembe mangapi?
18. Kurwa ana nazi 30. Doto ana nazi 40. Jumla wana nazi ngapi?
19. Mary ana shilingi 150. Rose ana shilingi 200. Je, wana jumla ya kiasi gani cha hela?
20. Said ana shilingi 350. Alitumia shilingi 250 kununua kalamu. Je, kilibaki kiasi gani cha hela?

**Kiambatisho Na 10: Arithmetic Skills**

Name of the Pupil..........................

Number of the Pupil.........................

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

## THE NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

## STANDARD TWO NATIONAL ASSESSMENT

**203 ARITHMETIC SKILLS**

Time: 1 Hour Monday, 23rd November 2015 Morning

## Instructions

1. This paper has **20** questions.
2. Answer **all** questions.
3. Write all answers in **pencil**.
4. Write your **name** and **number** on the first page.

| FOR ASSESSOR'S USE ONLY | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Question Number | Score | Assessor's Initials | Question Number | Score | Assessor's Initials | Question Number | Score | Assessor's Initials | Question Number | Score | Assessor's Initials |
| 7. | | | 7. | | | 13. | | | 19. | | |
| 8. | | | 8. | | | 14. | | | 20. | | |
| 9. | | | 9. | | | 15. | | | | | |
| 10. | | | 10. | | | 16. | | | | | |
| 11. | | | 11. | | | 17. | | | | | |
| 12. | | | 12. | | | 18. | | | | | |

Complete the pattern by filling in the missing numbers.

1. 6, 7, 8, _____, 10.

2. 15,14, 13, 12, _____.

3. 20, 22, 24, _____,28.

4. 60, _____, 80, 90,100.

5. 55, 60, _____, 70, 75.

Find out the answers:

6. 3 = ______.

7. 15+ 4 = ______.

8. 26+ 5 = _______.

9. 34 + 18 = _______.

10. 50 shillings + 100 shillings =_______ shillings.

11. 7 – 2= _______.

12. 18 – 6 = _______.

13. 24 – 9 = _______.

14. 45 - 17 = _________.

15. 500 shillings - 250 shillings =__________shillings.

16. In a class there are 7 boys and 8 girls. How many pupils are in that class?

17. A farmer has 19 mangoes. She gives her friend 10 mangoes. How many mangoes have remained?

18. Kurwa has 30 coconuts. Doto has 40 coconuts. How many coconuts do they have all together?

19. Mary has 150 shillings. Rose has 200 shillings. How much money do they have?

20. Said has 350 shillings. He used 250 shillings to buy a pen. How much money was left?

**Kiambatisho Na 11: Dodoso la Mwalimu Mkuu**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**UPIMAJI WA STADI YA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU**

**DODOSO LA MWALIMU MKUU WA SHULE**

**Jina:**_______________________________________________

**Shule unayoongoza:**________________________________

1. (a) Ni walimu wangapi wanaofundisha stadi za KKK?
_______________________________________________.

   (b) Kati ya waalimu hao wangapi ambao wamepata mafunzo ya stadi ya Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) katika shule yako?

_______________________________________________.

2. Shule yako ina jumla ya wanafunzi wangapi?

   (a) Darasa la Kwanza _________________________.

   (b) Darasa la pili _____________________________.

3. (a) Je unavyo vitabu vya kufundishia KKK katika shule yako?
____________________________________(Ndiyo/Hapana).

   (b) Je vitabu hivyo vinatosheleza kwa kila mwanafunzi?

_______________________________________________

4. (a) Je, una jumla ya mikondo mingapi kwa kila Darasa?

_______________________________________________

(b) Je, kila mkondo unakuwa na wanafunzi wangapi?

______________________________________________

5. Idadi ya madawati yaliyopo yanatosheleza kwa kila mwanafunzi?

______________________________________________

______________________________________________

6. Ni vifaa gani vinavyohitajika katika kumwezesha mwanafunzi kuelewa stadi za Kusoma Kuandika na Kuhesabu.

______________________________________________

7. Shule yako ina Muhtasari wa KKK?

(a) ____________________(Ndiyo/Hapana)

(b) Kama haupo umefanya mikakati gani ya kuupata?

______________________________________________

______________________________________________

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**UPIMAJI WA STADI YA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU**

**DODOSO LA MSIMAMIZI MKUU**

**Jina:**________________________________________

**Shule unayofundisha:**____________________________

**Shule unayosimamia:**____________________________

1. Je, unafundisha Kusoma , Kuandika na Kuhesabu katika darasa la 1 au la 2? _________(Ndiyo/Hapana)

2. Je, umeshawahi kupata mafunzo ya stadi ya Kusoma Kuandika na Kuhesabu?

   (a) Kama jibu ni ndiyo onesha mafunzo yalitolewa wapi na kwa muda gani.

   ________________________________________

   ________________________________________

   (b) Mafunzo hayo yalikupa maarifa na ujuzi gani?

   ________________________________________

   ________________________________________

3. Kituo ulichosimamia upimaji wa Darasa la Pili 2015 kilikuwa na wanafunzi wangapi?

   ________________________________________________

4. Je, kuna wanafunzi walioshindwa kufanya upimaji huu? Kama wapo waorodheshe majina yao na sababu za kushindwa kufanya upimaji.

| Na | Jina | Sababu za Kushindwa Kufanya Upimaji |
|---|---|---|
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| 5. | | |
| 6. | | |
| 7. | | |

5. Ni changamoto zipi zilijitokeza katika shule uliyosimamia?

(a) Eleza changamoto hizo kwa kifupi.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

(b) Je, changamoto hizo ziliathiri kwa namna gani upimaji huo?

______________________________________________

______________________________________________

(c) Eleza namna ulivyozitatua changamoto hizo.

______________________________________________

**Kiambatisho Na 13: Dodoso la Mwalimu (Msimamizi)**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**UPIMAJI WA STADI YA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU**

**DODOSO LA MWALIMU(MSIMAMIZI)**

**Jina:**___________________________________________

**Shule unayofundisha:**________________________

**Shule unayosimamia:**________________________

1. Je, unafundisha Kusoma , Kuandika na Kuhesabu katika Darasa la 1 au la 2? _________(Ndiyo/Hapana)

2. Una uzoefu wa muda gani katika kufundisha Darasa la 1 au 2?____________(Onesha Miaka).

3. Je, umewahi kupata mafunzo ya KKK? ____________ (Ndiyo/Hapana)

   Kama jibu ni ndiyo onesha mafunzo yalitolewa wapi na kwa muda gani.

   ____________________________________________________

   ____________________________________________________

4. Je, ni kwa kiasi gani wanafunzi wameweza kusoma kwa ufasaha na kujibu maswali ya kusoma kwa usahihi?

   ______________________________(kikubwa,wastani,kidogo).

5. Je, Darasa ulilosimamia lina jumla ya wanafunzi wangapi?

6. Muda uliopangwa wa upimaji kwa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu ulitosheleza?

_______________________________________________(Ndiyo/Hapana)

Kama jibu ni hapana toa mapendekezo yako.